Toleo Maalum la Mwezi wa Ramadhani

Ramadhani na Ibada

"Kwa yakini kila kitu kinakuwa na mlango wake, na mlango wa ibada ni saumu"

uk. 8



Maana ya Saum

...shabaha na kusudio hasa la saumu ni kupata Ucha-Mungu....

uk. 2



Ramadhani na Maombi

Ninajibu dua ya muombaji anaponiita Mimi...

uk. 11

Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 81 No. 221 | SHAB.-RAMADH.1442AH | APRILI 2021 | SHAHADAT 1400 HS | BEI TSH. 500/=

Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa mwongozo kwa watu, na Ishara zilizo wazi za mwongozo na kipambanuzi. Basi miongoni mwenu atakayeuona mwezi, afunge saumu, na mwenye kuwa mgonjwa au yumo safarini, basi atimize hesabu katika siku zingine. Allah Huwatakieni yaliyo mepesi wala Hawatakieni yaliyo mazito, na pia (Huwatakieni) mtimize hesabu na kumtukuza Allah kwa kuwa Amewaongozeni, na ili mpate kushukuru. **Al Baqara (2:186)**

Fiqh katika Saumu ya Ramadhani



- **Kuuona Mwezi**
- **Mwisho wa Kula Daku**
- **Saumu ya Mgonjwa na Msafiri**
- **Watoto na Ramadhani**
- **Kupiga Mswaki katika Saumu**

uk. 9

Baraka na Ubora wa Ramadhan

Allah Anasema akieleza ubora na baraka za saumu kuwa:

"*Mwezi wa Ramadhan, ambao humo imeteremshwa Kurani kuwa mwongozo kwa watu na dalili zilizo wazi na mwongozo na ishara ipambanuayo. Na miongoni mwenu atakayeuona mwezi huu basi afunge saumu. Na awaye mgonjwa au katika safari basi alipe katika siku zingine. Allah huwatakieni yaliyo mepesi wala hawatakieni yaliyo mazito, na pia huwatakieni mtimize hesabu na kumtukuza kwa sababu amewaongozeni, ili mpate kushukuru.*" (2:184-186).

Ameeleza Mtume[saw] ubora na fadhila za mwezi wa Ramadhani katika hadithi zifuatazo-:

"*Laiti Kama watu wangelijua fadhila za Ramadhani basi Ummati wangu ungelitamani kuwa (mwezi wa) Ramadhani ungepanuka na kuwa (Ramadhan kwa) mwaka mzima, hapo mtu mmoja aliuliza kwamba, ewe Mjumbe wa Allah! Kuna fadhila gani za Ramadhani? Yeye[saw]. Akajibu: kwa yakini Pepo inapambiwa kwa ajili ya Ramadhani toka mwanzo wa mwaka hadi mwishowe.*" (Muújamul Kabir J.22.UK.388)

Nabii wa Allah[saw] Alisema akieleza ubora wa Ramadhani: *Atakaefunga Ramadhani hali ya kuamini na kutaraji thawabu atasamehewa dhambi zake zilizo tangulia*" (Bukhari na Muslim)

Mtume Mtukufu[saw] alisema: "*Saumu na Qurani zinamuombea mja, saumu itaomba hivi kuwa, E Mola wangu! Mimi nimemzuia kula na matamanio mengine mchana kutwa basi upokee maombezi yangu juu yake, na Qurani itasema, mimi nimemzuia kulala usiku (yaani aliendelea kusoma Qurani) basi ukubali maombezi yangu kumhusu yeye, basi maombezi yao (ya Quran na ya saumu) yatapokelewa.*" (Al-Baihaqi na

Endelea uk. 4

Ramadhan na Qur'an



Allah Anasema:

"*Mwezi wa Ramadhan, ambao humo imeteremshwa Kurani kuwa mwongozo kwa watu na dalili zilizo wazi na mwongozo na ishara ipambanuayo.*" (Suratul Baqarah 2:186)

Kisha Anasema: *Na (soma) Qurani alfajiri. Hakika kusoma Qurani alfajiri kunakubaliwa (sana).* (Sura Bani Israiil 17:79)

Bwana wetu mpendwa Mtume[saw] anasema: "*Saumu na Qurani*

Endelea uk. 5

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Funga ya Ramadhani

Amri ya kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani unapatikana katika Qur'an tukufu:

"Enyi mlioamini mmefaradhishiwa kufunga Saumu kama walivyo faradhishiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Allah" (2:183)

Kama yalivyo mafundisho ya Islam kuna falsafa na faida katika kila fundisho. Na Islam pia inachukua njia ya katikati kila fundisho. Ingawaje amri imetoka ya kufunga saumu wapo waliosamehewa. Kwa mathalani mtu mgonjwa, msafiri, mama anayenyonyesha, mtoto, mzee ambaye hawezi kuhimili vishindo vya saumu lakini katika ruhusa hiyo hali ikiwa nzuri inabidi kufunga siku hizo ambazo hukufunga. Kwa masikitiko makubwa wapo ambao katika jazba zisizo uhusiana na mbora wa manabii ambaye ni ***fii rasuulihi uswatun hasana*** katika maisha yake aliyaeleza hayo kinagaubaga, ukifunga wakati unaumwa unafuata mfano wa nani?

Funga ya Ramadhani ni tangazo adhimu kwa ajili ya masikini. Katika mwezi huo kama vile mwezi na jua vinaangaza kwa wote masikini na tajiri, hali kadhalika. Mwezi wa Ramadhani hata yule mwenye hoteli kubwa nchini anashinda njaa! la msingi sio kwamba hana chakula bali ni amri ya Jalia. Kama unaweza kuacha kitu cha halali kwa sababu ya Jalia unawezaje kugusa kila ambacho amekataza Allah.??

Moja ya tatizo linalokabili viongozi ni daima kusema wasiyoyatenda. Kwa sababu ya kutambua kuwa hakuna anayekuona Ramadhani inakufundisha kumaizi kuwa unapokuwa mmoja yupo wa pili yaani Allah. Utamaduni huo ukikuingia utafanya kazi kwa bidiii na huku ukitambua kuwa kesho kuna maswali ya kujibu.

Binadamu anasahau kwa haraka shabaha ya kuumbwa kwake. Tumeumbwa ili kumuabudu Allah. Ramadhani inatufikisha kwenye kiwango cha juu cha kumuabudu Allah. Utamaduni unaotakiwa kuendelezwa mwaka mzima. Allah Atujaalie kutofautisha kati ya **kufunga saumu** na **kushinda njaa**.

Maana ya Saumu

Saum ni neno la kiarabu ambalo linamaanisha kuwa kujizuia na kuwazuia wengine.

Neno la saum limetumika ndani ya Qurani Tukufu kwa maana ya kujizuia kusema pia kama ilivyobainishwa katika aya 27 ya sura Maryam kwamba na ndani ya aya hii neno "saum" lina maanisha kujizuia kusema.

Imam Nauwi anaandika juu ya istilahi ya kisaumu kwamba; *kujizuia kula, kunywa n.k. kwa muda maalum kisha kwa masharti maalum, huitwa saumu sawa na istilahi ya Kiislam.*

Tukizingatia maana ya lugha na ya kiistilahi pamoja na aya za Qurani Tukufu na hadithi za Mtume Mtukufu^{saw} tutasema maana kamili ya saumu ni hii kwamba; Muislamu, mwenye akili timam, aliyebalehe na aliye mzima wa afya, ajizuie kula na kunywa, tendo la ndoa, na maovu yote, toka mapambazuko ya Al-Fajiri hadi kuzama kwa jua kisha ajishugulishe na ibada mbali mbali kama vile kusali sala tano kwa kuzingatia masharti, kusoma Qurani Tukufu, kuwasaidia maskini na wenye shida kisha ajidhibiti nasfi yake na kila kiungo cha mwili wake kipate kuhisi kuwa kimepata mabadiliko maalum ndani mwake kwa sababu ya saumu. kila sehemu ya mwili wa mtu, itakapopata mabadiliko basi nafsi ya mtu husika itakuwa na mafanikio, maendeleo na mapinduzi makubwa yanayoitwa kujirekebisha nafsi, ambayo ni Taqwa sawa na istilahi ya Qurani na shabaha na kusudio hasa la saumu ni kupata Ucha-Mungu.

Saumu katika Dini Zilizotangulia



Kufunga saumu si jambo lililoanzishwa na Islam au Mtume wa Islam bali ni ibada iliyotekelezwa na nyimati za mitume wa Allah waliopita kabla ya Mtume Muhammad^{saw}. Pia, Allah Mwenyewe Anasema:

"Enyi mlioamini mmefaradhishiwa kufunga Saumu kama walivyo faradhishiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Allah" (2:183)

Ingawaje kuna tofauti kwenye sura ya kidhahiri kati ya saumu za Kiislam na saumu za Dini zilizotangulia lakini mambo ya msingi yako sawa. Kuna Hadithi ya Mtume wetu mtukufu iliyopokelewa na hazrat Amr bin Al-Aasi^{ra}. Kwamba; *"Tofauti baina ya saumu zetu na za watu wa Kitabu ni kula daku. (yaani Waislamu wanakula daku na watu wa Kitabu hawali daku)."*

Khalifa wa pili wa Seyyedna Ahmad^{as} hazrat Mirza Bashir ud din Mahmood Ahmad^{ra} anasema;

"Hakuna shaka kwamba kulikuwa na tofauti kwenye sura (ya kidhahiri) ya saumu na ile tofauti inaonekana hadi leo. Kulikuwepo saumu ambazo zinaitwa za "Wisal" kuwa hawali daku kati ya saumu. Walikuwa wanafuturu jioni katika saumu za namna hii na kufunga saumu ya pili bila ya kula daku na kuendeleza saumu (kwa siku mbili mfululizo).

Pengine kulikuwa na saumu za namna hii kwamba walikuwa hawafuturu na kufunga siku tatu, siku nne hata siku tano mfululizo.

Kuna aina za saumu ambamo watu waliruhusiwa kula chakula chepesi lakini walikatazwa kuvitumia vyakula vigumu(vizito) kama ni saumu ya mabaniani na ya Wakiristo.

Inajulikana kama kwaida juu ya saumu ya mabaniani kwamba saumu yao inakuwa hivi kuwa hawali kitu kilichopikwa na moto pasipo hiki kama wanakula kilo kadha ya embe, ndizi na chungwa basi saumu yao haiharibiki, wanaweza kula cho chote pasipo chapati na mboga (kilichopikwa na moto).

Kisha kuna saumu rahisi zaidi zinazopatikana katika Wakiristo wa Katoliki, hawa pia watakuwa wameanza saumu za namna hii kwa msingi Fulani wa Dini au walipokea riwaya ya mwanafunzi yeyote. Saumu yao inakuwa hii kwamba hawali nyama. Wao kama wanachemsha viazi au kutengeneza mboga ya mamungu'nya na kula pamoja na chapati basi saumu yao haibatiliki ila kama kipande cha nyama kinaingia tumboni mwao basi saumu inabatilika hivyo basi kuna hitilafu zinapatikana baina ya Mataifa tofauti tofauti kuhusu saumu. (Tafsire Kabir J.2.UK.370-371)

Imeandika ndani ya Incyclopedia Britanica kuhusu saumu kwamba: *"It would be difficult to name any religious system of any description in which it is wholly unrecognized."*
(ni vigumu kutaja mfumo wa dini yoyote ya namna yoyote ambamo kwa ujumla saumu haitambuliki)

Hakuna Dini isiyoleta amri ya kufunga saumu, bali amri ya kufunga saumu inapatikana katika kila Dini. Hazrat Mirza Bashir ud din Mahmood Ahmad^{ra}. Anasema akifafanua zaidi somo hili kwamba:

"Imeandikwa ndani ya Taurati kwamba, hazrat Mussa^{as} alipoenda kwenye mlima wa Toori(Sinai) basi alifunga saumu ya siku 40 na hakula wala kunywa ndani ya siku hizi. Hivyo imeandikwa: "basi yeye (yaani Mussa^{as}.) alikaa pale usiku na mchana kwa siku 40 mbele ya Allah na hakula chapati wala hakunywa maji." (Kutoka 34:28)

Hali kadhalika tunapata kujua kupitia kitabu cha Ahbar, Mlango wa 16 na mstari wa 29 kwamba Wayahudi walilazimishwa kufunga saumu moja ya tarehe 10 ya kila mwezi wa 7 hivyo Wanawaisraeli walikuwa wanafunga saumu hizi daima na Manabii wa Wana wa Israeli pia walikuwa wanawaagiza juu ya hilo. Hazrat Dawood^{as} anasema katika Zaburi:

Endelea uk. 3

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Maana ya Saumu

Kutoka uk. 2

"Mimi nilijifunika na blanketi wakati walipokuwa wanaumwa na kujitaabisha kwa kufunga saumu." (Zaburi 35:13)

Yasaya Nabii anasema: Tazameni! Mnafunga saumu kwa lengo hili kwamba mugombane na mupigane kwa utundu basi hamfungi saumu ya namna hii kwamba sauti yenu isikilizwe kwenye ulimwengu wa juu. **(Isayah 58:4)**

Danieli Anasema: "Nilimuelekea Allah na kumtafuta Yeye nikiwa nimefunga na kujifunika na blanketi na kukaa kwenye udongo. **(Danieli 9:3)**

Tukitazama Ukiristo baada ya Uyahudi basi tunakuta humo uthibitisho wa kufunga saumu, hivyo Injili inatuelezea kumhusu hazrat Masih[as] kwamba yeye alifunga saumu ya siku 40, mchana na usiku. Imeandikwa kwenye Mathayo:

Na hatimaye alipata njaa baada ya kufunga kwa siku 40, mchana na usiku. **(Mathayo 4:2)**

Hivyo hazrat Masih[as]. aliwaagiza wanafunzi wake kuwa;

Mnapofunga saumu basi msiwe na nyuso za kusononeka jinsi wafanyavyo wale wanaojionesha, wao wanageuza nyuso zao ili watu watambue kuwa wamefunga, ninawambieni kweli kweli kwamba wao wameshapata ujira wao. Ufungapo saumu paka mafuta kichwani mwako na kuosha uso ili sio watu bali Baba Yako aliyejificha, Akujue kuwa wewe ni mfunga saumu ndipo Baba Yako Anayejua siri Atakulipa. (Matayo. Mlango 6.Msitari 16-18)

Hali kadhalika safari moja, Wanafunzi waliposhindwa kutoa pepo mbaya basi Wanafuzi wake (Masih[as]) walimuuliza kwa upweke kwamba kwanini hatukuweza kuitoa ndipo Aliwaambia kuwa:

Aina hii (ya pepo) haitoki kwa namna yoyote nyingine ila kwa dua na saumu. (Marko.Mlango.9. Msitari28-29)

Yaani sifa za ubora wa Kiroho zinapatikana kikamilifu kwa saumu na maombi tu…

Tunapochunguza Dini ya Ubaniani baada ya Ukiristo na Uyahudi basi tunakuta kwao, saumu ya namna kadhaa na kuna masharti tofauti tofauti na vigezo juu ya kila aina ya saumu ambazo zimeelezwa ndani ya kitabu chao kiitwacho "Dharam Sindhu". Saumu za Mabaniani na za Jainmat zimeelezwa katika Incyclopedia Britanica pia, na imeandikwa kuhusu Dini ya Zorosta kwamba Zartasht aliwaagiza watu wake juu ya kufunga saumu. (Incyclopedia Britanica J.9.chini ya neno Fasting)

Kwa kifupi, saumu ni njia ile ya maendeleo ya Kiroho inayoonekana katika Dini zote kwa jumla. Na nyimati zote ziliendelea kupata baraka kupitia saumu. (Tafsire Kabir.J.2.UK.371-373)

Fadhila na Ubora wa Saumu

Mtume wetu Mtukufu[saw] alisema akieleza baraka za kufunga saumu kwamba:

1. *Kufunga ni kinga ya Moto kama vile kinga ya mmoja wenu katika vita.* (Musnad Ahmad na Nasaiy)

2. Kisha anasema Mtume Muhammad[saw] *"Atakae funga siku moja katika njia ya Allah, Allah atamwepusha kwa utukufu wa siku hiyo uso wake na joto la moto wa Jahannam umbali wa miaka sabini."* (Musnad Ahmad, Nasaiy, Ibn Majah na Tirmidhi)

3. Hazrat Abu Umamah anasimulia kuwa: *"nilimuomba Mtume[saw] kwamba aniamuru amri ambayo kwayo Allah Atanifaidisha, alisema (Mtume[saw]) juu yako ni kufunga saumu kwani hakuna mfano wake."* (Al-Nasaiy)

4. *"Saumu ni nusu ya subra na subra ni nusu ya Imani."*

Dawa kubwa na ya msingi kabisa kwa ajili ya kuondoa matatizo mengi na shida nyingi za jamii yetu ni kushika subra na kama mtu yeyote anatabia hii basi taabu nyingi zinamuondoka. Tabia ya kushika subra inamuongoza mtu kwenye kujitolea na kutoa dhabihu na tabia hii inaondoa kiburi na kujivunia bure na subra inazalisha ndani ya mtu husika tabia ya kuvumilia na upole na kufunga saumu ni mazoezi bora zaidi ya kupata tabia ya subra na utulivu.

Hazrat Hakiim Maulana Noor Uddin r.a Khalifa wa kwanza anasema:

"bila shaka, hakuna ibada yenye fadhila na bora zaidi kuliko saum kwa ajili ya kufuta giza za mwilini na hakuna kitu kikubwa zaidi kuliko saumu kwa ajili ya kupata nuru na ufunuo wa Kiungu." (Khutbate Noor, UK.230)

Dhambi ya Kuacha Saumu ya Ramadhani

Mtume Mtukufu[saw]. alisema akieleza dhambi ya kuacha saumu ya Ramadhani kwamba:

1. *Aliyeacha kufunga saumu siku moja ndani ya Ramadhani bila ruhusa Aliyompa Allah basi haimtoshi hata kama anafunga (baadaye) saumu za mwaka mzima.* (Abu Dawood, Kitab us Siyam)

2. Riwaya nyingine inasema hivi;

"Aliyeacha kufunga saumu siku moja bila udhuru na ugonjwa basi haimtoshi hata kama anafunga(baadaye) saumu za mwaka mzima." (Tirmizi. Abwab us saum)

Ningependa kuweka mbele ya wasomaji watukufu usemi wa seyyedna Ahmad[as], yeye anasema:

"Kama Allah Angependa Asingeweka vikwazo na mipaka kwenye umati huu sawa na nyimati zingine, lakini Ameweka mipaka kwa ajili ya faida tu. Hili ni jambo la msingi kwa mtazamo wangu kwamba, mtu anapomuomba Allah kwa ukweli na uaminifu kamili kwamba Unijaalie nisikose (baraka za) mwezi huu basi Mwenyezi Atamjaalia na baraka zake na kama mtu akipata kuumwa katika hali ya namna hiyo basi ugonjwa huu utakuwa rehema kwake kwani kila kitendo kinategemea nia. Mumini anatakiwa ajithibitishe kwa dhati yake kuwa yu shujaa katika njia ya Allah. Mtu anayekosa kufunga saumu lakini alikuwa na nia na moyo wake ulikuwa unaumia kwamba laity ningekuwa mzima wa afya na kufunga saumu kisha moyo wake hulia kwa ajili yake basi malaika watafunga saumu mahala pake, ila yule mtu asiwe mwenye kutafuta udhuru basi Allah Atamjaalia asikose thawabu kamwe."(Al-Badri J.1 tarehe 16 January 1903 kupitia Tafsiri ya Hazrat Masihe Maud[as] J.2.UK.262.Chapa mpya)

Kisha anasema pengine Hazrat Ahmad[as]. Akieleza hali yake kwamba:

"Hali yangu iko hivi kwamba, naacha kufunga ninapokaribia kufa tu. Tabia yangu haipendi kabisa kuacha kufunga saumu. Siku hizi ni zenye mibaraka na siku za kushuka kwa fadhila na rehema ya Allah Mtukufu".

Umri wa Kufunga Saumu

Hazrat Khalifatul Masih wa pili wa Seyyidna Ahmad[as] anasema: *"Inapaswa kukumbuka jambo hili kwamba, sheria (ya dini) imewakataza Watoto wenye umri mdogo kwa kufunga saumu lakini inatakiwa kuwazoesha kufunga saumu kadhaa wanapokaribia kwenye kupata ubalehe. Sawa na kumbu kumbu langu, hazrat Masihe Maud[as] aliniruhu kufunga saumu ya kwanza katika umri wa miaka 12 au 13. Lakini baadhi ya wapumbavu wanawalazimisha Watoto wenye umri wa miaka 6 au 7 kwa ajili kufunga saumu na kudhani watapata thawabu yake. Hii si shuguli ya thawabu bali ni dhulma kwani umri huu ni umri wa kukua ila kuna sehemu ya umri inayokaribia kwenye siku za kupata ubalehe na muda wa kufaradhishwa kwa saumu unakuwa umekaribia, basi wakati ule ni lazima tuwazoeshe na saumu. Inapochunguzwa ruhusa na sunna ya Hazrat Masihe Maud[as] basi tuwazoeshe kidogo kidogo kwenye umri wa miaka 12 na 13 na kila mwaka walazimishwe kufunga saumu kadhaa hadi wafike umri wa miaka 18 ulio ni umri wa balehe, kuhusu saumu mbele yangu. Hazrat Masihe Maud[as] aliniruhu kufunga saumu moja tu katika mwaka wa kwanza."* (Tafsire Kabiir J.2.UK.385)

(Al-Hakam J.5.Tarehe 24 Feb.1907)

Saumu na Afya ya Kimwili

Bwana wetu Mtume Mtukufu[saw] alisema; *"fungeni saumu mtapata afya"* (Al-Kamil, 3:227 na Zakhiratul Huffaz Le Ibne Al-Qaisarani)

Hatuna shaka kwamba kufunga saumu ni ijtihada ya Kiroho na busara ya mtu husika inaongezeka kwa saumu lakini kidhahiri pia binadamu anazoea kuvumilia na shida na taabu. Ama faida za saumu kuhusu afya za binadamu pia zimethibitishwa na wanasyansi na kwa siku ya leo jambo hili ni la kwaida tu linaloeleweka na watu wengi hasa wasomi, na wanafahamu vyema kuwa kuna sumu hatari kabisa zinazotoka kutoka mwilini mwa binadamu wakati anaposhinda na njaa kwa muda Fulani, unene unapungua n.k.

Mtume wetu Mtukufu alisema:

"kuna zaka ya kila kitu, na zaka ya mwili ni saumu"

Hazrat khalifatul Masih wa pili anasema akieleza somo hili kwamba; *"Hii ndio maana ya "laallakum Tattaqoon" kwamba mpate kujilinda na shari za dini na za kidunia. Msikose heri na baraka ya dini au msipata madhara ya kiafya kwani muda mwingine saumu zinakuwa sababu ya kulinda na maradhi ya namna kadhaa.*

Utafiti wa siku hizi zinathibitisha kuwa uzee au udhaifu unatokea kwa sababu hii tu kwamba usaha na ute wa aina fulani unazidi mwilini mwa mtu nao unasababisha maradhi au mauti, baadhi ya wapumbau wamezidi kiasi hiki kwenye mtazamo huu kwamba siku ambamo tutafaulu kufuta kabisa ule ute na usaha basi siku hiyo mauti pia itaondoka. Ingawa wazo hili ni la upumbavu lakini hakuna shaka ndani yake kwamba uchovu na udhaifu unazalika mwilini kwa sababu ya kukusanyika kwa usaha kwa wingi na saumu inafaa sana kwa ajili yake. Nami mwenyewe nimeshuhudia kwamba saumu zinapofungwa wakati wa afya nzuri basi ingawa tunahisi taabu Fulani ndani ya Ramadhani lakini tunajisikia nguvu mpya mwilini na bashasha na furaha baada ya Ramadhani." (Tafsire Kabiir J.2.UK.375)

Khalifa wa zama Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba] anasema: *"Saumu hizi za siku chache, si tu kwamba ni chanzo cha kupata ridha ya Allah bali zinafaa kwa ajili ya afya ya miili yetu, na huu ndio ukweli uliothibitika kwamba, inatakiwa tuwe na muda Fulani ndani ya mwaka ambamo mtu ale chakula kwa kiasi kidogo tu, basi tunaendelea kupata manufaa mara mbili ya hili, afya ya mwili na ridhaa ya Allah pia."* (Kutbate Masroor J.1.UK.423)



"Saumu ni nusu ya subra na subra ni nusu ya Imani."

Baraka na Ubora wa Ramadhani

Kutoka uk. 1

Mishkat Kitab us Saum)

Bishara hii ni kubwa mno iliyoelezwa ndani ya hadithi hii ya bwana wetu Mtume Mtukufu[saw] kwa ajili ya wale watu ambao hufunga saumu ndani ya mwezi huu Mtukufu kwa kuzingatia masharti na adabu zake kisha wanajishugulisha katika kusoma Kitabu cha Allah na kukifahamu maana yake na kuyafuata maamrisho yake kwa moyo mkunjufu. Mzuri ulioje usemi huu wa seyyedna Ahmad[as]: *"Watakaoheshimu Qurani wataheshimiwa mbinguni"* (Kasht-e-Nuh)

Bwana wetu mpendwa Mtume Mtuku[saw] Anasema katika hadithi nyingine iliyo ni maarufu sana kuhusu baraka za Ramadhani kuwa: *"Inapokuwa usiku wa kwanza wa Mwezi wa Ramadhani Mashetani hufungwa na Majini wakorofi nao, hufungwa pia Milango yote ya moto, na hufunguliwa milango yote ya pepo. Hutangaza mtangazaji (malaika) kwa kusema: Ewe unaetaka kheri elekea katika kheri hiyo, na Ewe mwenye kutaka shari acha shari hiyo, Allah huwa anawaacha huru na moto. Na maneno haya husemwa kila usiku"* (Tirmidhi).

Hazrat Mirza Tahir Ahmad[rh] Anasema akieleza maana halisi ya hadithi hii kwamba; *"Swali ni hili kwamba mradi wa milango hii ni nini hata kama ni milango ya mbinguni au peponi na milango ambayo hufungwa ni milango gani ya Jahannam na minyororo ya aina gani ambayo kwayo hufungwa mashetani? Je kuna hali ya kawaida ilielezwa au kuna maana maalum ambayo inahusiana na baadhi ya wakati tu na hali hiyo haina uhusiano na dunia nzima kwa jumla?*

Ama mwezi wa Ramadhani huja kwa maana yake ni haya kwamba, mwezi wa Ramadhani huja na baraka popote pale unapoingia (mioyoni mwetu). Mtume Mtukufu[saw] alikuwa mwana lugha na mwenye kujua sana nukta fasihi za kielimu, na hakuna aliyeshuhudia nukta fasihi za Lugha kwa yeyote mwingine min ghairi yake Yeye[saw]. Baada ya kitabu cha Allah, hivyo Mtume[saw] aliweka mwanzoni mwa hadithi hii funguo wa kuifahamu. Yeye[saw] alisema, ***iza dakhala shahru Ramadhana****, kwamba unapoingia na popote pale utakapoingia utaleta hali hiyo na maana yake ni hii kwamba, Ramadhani itakapoingia popote kwa masharti yake yote basi itakuwa sababu ya kumletea binadamu baraka zake waila Ramadhani si kitu Fulani kinachoweza kuingia mijini au nchini bali inaingia ndani ya dhati ya mtu. Mradi wake ni huu kwamba, mwezi wa Ramadhani uingiapo ndani ya dhati ya mtu yeyote basi mabadiliko mema yatazalika ndani ya ulimwengu wake, mabadiliko yatapatikana kwenye mbingu na ardhi yake, inamaana mtu anayejiweka chini ya Ramadhani basi Ramadhani itaingia ndani yake yule mtu kwa baraka zake zote, hali kadhalika milango yote inayopatikana kwenye ulimwengu wake itafunguka na kufungwa milango yote ya Jahannamu yaani milango ya rehema ya Allah itafunguliwa kwake na shetani wake atafungwa minyororo, hii ndio maana ya asili ya hadithi hii. Hivyo tunapotafakari zaidi kwa namna hii basi hakuna ugumu unaopatika kujua kwamba milango ile ni ipi?*

Ama dhati ya binadamu, kuna hisia (au milango ya fahamu) tano, zinazoitwa hisia tano (za maarifa) yaani hisia ya kunusa, hisia ya kusikia, hisia ya kuona,hisia ya kuonja, hisia ya kugusa kisha kuna njia za namna mbili zingine (njia za haja), alizopewa binadamu kwa ajili ya kuingia au kutoka….mtu amejaaliwa na njia za namna ambazo zina uwezo wa aina zote mbili, inaweza kuingia humo kitu au kutoka humo, nazo zinaumuhimu mkubwa kwenye Maisha ya binadamu na zikihesabiwa hizo basi milango ya ulimwengu wa mtu inakuwa saba. (na mbingu saba pia zinamilango saba). Hii ndio baraka ya Ramadhani na njia moja tu ya ibada inayoweka vikwazo juu ya milango hiyo saba na hamwezi kuwaza ibada nyingine yoyote inayotawala kikamilifu nguvu hizo za mtu na njia hizo zote.

Hivyo basi maana yake ni hii kwamba mtu anapoweka nguvu hizi au njia saba chini ya ridhaa ya Allah kana kwamba humfungulia kwake milango saba tokea mbinguni. Idadi ya saba ni alama (symbolic) na namna moja ya kueleza na muradi wake ni huu kwamba mtu anayejiweka nguvu zake zote chini ya ridhaa ya Allah Mtukufu basi nguvu zote za Allah Mtukufu humfungulia milango ya rehema. Mtu wa namna hiyo anapofunguliwa milango ya mbinguni kwa fadhila za Allah, basi haziwi saba bali zinakuwa nyingi zisizohesabika, hivyo ni jukumu la mumini, anapoingiza ndani mwake Ramadhani kwa baraka zake basi afungue kila cha kwake (ajiweke wazi) kwa ajili ya Allah na kufunga kabisa kwa ajili ya shetani ndipo milango ya rehema yaani ya fadhila za Allah zinafunguka ambazo ni nyingi kuliko saba, ambazo haziwezi kuzihesabika (bila shaka tunweza kusema kuwa idadi kamili ni 7). Mumini anapouweka ulimwengu wake mbele ya Allah basi Ulimwengu wa Allah unaanza kumshushia rehema kwa pande zote, hii ndio maana ya hadithi hii ya Mtume[saw] aliyoisema akituelezea baraka za Ramadhani. (Khutbate Tahir J.2.UK.331-334)

Pia ndani ya mwezi huu ndimo Qur'an iliteremshwa kutoka katika Lawhum Mahfuudh ilaa samaai dduniya (Kutoka Lawhim Mahfuudh mpaka mbingu ya kwanza). Hivyo kwa ubora wa Qur'an basi inaunyanyua mwezi huu na kuwa bora kama Allah alivyosema katika Qur'an kuwa-: *"Mwezi wa Ramadhaan ni mwezi ambao imeteremshwa Quraan ili iwe uongozi kwa watu na hoja na upambanuzi (Baina ya haki na batil)"* (Qur'an Baqarah,2:185)

Hazrat Mirza Masroor Ahmad[atba], Khalifa wa Tano wa Seyyedna Ahmad[as] anasema: *"Ramadhani ni mwezi wenye mibaraka kwa ajili ya wale watu ambao wanataka kumuabudu Allah Mtukufu kwa kujihalisisha na kufanya ibada. Huu ni mwezi wenye mibaraka kwa ajili ya wale wanaotaka kufanya wema ule na kuutenda ulioamrishwa na Allah Mtukufu wakifuata maagizo ya Allah Taalah na kuachana na kila ubaya ulioamrishwa na Allah kuuacha, bali wanaviacha vilivyo halali pia kwa muda maalum kwa ajili ya amri ya Allah Mtukufu."* (Khutbate Masroor J.2.UK. 739-740)

Shabaha na Kusudio la Ramadhani

Mungu Mwenye Enzi Anasema ndani ya Qurani Tukufu akieleza kusudio la kufunga saumu ya Ramadhani kuwa:

1. Ili mpate kujilinda na upungufu wa kikhulka na ukosoro wa kijamii kwa kumuogopa Allah.
2. Ili mudhihirishe ukubwa wa Allah Mtukufu sawa na mwongozo Wake (kwani Amewaongozeni).
3. Ili mpate kumshukuru (Allah)

Mtume Mtukufu[saw] alisema kuhusu Ramadhani: *"Atakayesimama Ramadhani ilhali ya kuamini na kutaraji thawabu (Kwa kujichunguza hasa) Allah Atamsamehe dhambi zake zilizotangulia"* (Bukhari na Muslim)

Hazrat Maulana Noor Uddin[ra]., Khalifa wa kwanza wa seyyedna Ahmad[as]. anasema akinuku hadithi hii ya Mtume[saw] kwamba: *"Badhi ya watu wanasema kwamba, matumizi (ya nyumbani) hua yanaongezeka ndani ya Ramadhani, ilhali jambo hili ni la uwongo. Ukweli ndio huu kuwa wale watu wameghafilika na roho ya saumu. Wanakula sana daku na kushiba mno kiasi hiki kwamba hadi mchana wanapiga mbweu kutokumeng'enya chakula na kama muda umefika wa kumeng'enya chakula kwa taabu tu wakati wa kufuturu basi tena wanashiba vibaya na vyakula vizuri vizuri na kujaza mno tumbo kiasi kwamba wanaanza kupata usingizi juu ya usingizi na uvivu mkubwa kama wanyama wa porini. Hawazingatii kuwa saumu ni kujitahidi (mazoezi) si kwamba tufanye matumizi makubwa kuliko awali na kula kwa kujaza sana tumbo. Kumbukeni kwamba, Qurani Tukufu ilianza kushuka ndani ya mwezi huu na Qurani Tukufu ni nuru na mwongozo kwa ajili ya watu. Inatakiwa kutenda sawa na mwongozo wake. Uhuru na Upweke unazalika kwa saumu na njia za kupata utulivu katika shughuli za kidunia. Starahe hupatikana baada ya kifo au kwa kujilinda na maovu, hivyo faraja hupatikana kwa saumu pia na mtu anaweza kuwa Muttaqi na kupata ukaribu na Allah Mtukufu na kama watu wakikuuliza kwamba ukaribu wake unaweza kupatikana vipi kwa saumu basi sema, basi Mimi Niko Karibu, Ninajibu dua ya mwombaji anaponiomba…* (Al-Hakam 17 Nov.1907.uk.5.,Haqaiqul Furqan J.1.UK.307)

Seyyedna hazrat Masihe Maud[as]. anasema: *"Jambo ambalo ni nguzo la Islam nalo ni Saumu. Watu hawafahamu ukweli wa saumu…saumu sio hii tu kwamba (mfunga saumu) ashinde na njaa na kiu bali (saumu) ina ukweli wake na athari zake, inayojulikana kwa uzoefu. Na ni asili ya tabia ya binadamu kwamba kadri anavyopunguza kula basi hupata kujitakasa zaidi nafsi na nguvu za kupata kashifu (ufunuo wa Mungu) zinaongezeka."* (Tafsir Hazrat Masihe Maud[as] J.1.UK.258.Chapa mpya)

Jambo ambalo ni muhimu sana na la kutilia manani ni hili kwamba dini tukufu ya Islam inatusisitizia na kutilia mkazo juu ni nia ya mtu inayofanya kazi nyuma ya kila amali zake na Islam inaagiza zaidi juu ya kuiweka sawa nia na roho inayotumika wakati wa kufanya kitendo fulani bila kujali matendo, na Mtume Mtukufu[saw] ameshaeleza ukweli huu ndani ya usemi wake huu kwamba: *"kuna wengi wa wafungao saumu ambao hawapati ujira ila kiu tu, na wapo wengi ambao hukesha usiku (na kusali Tahajjud) lakini hawapati ujira zaidi ya kuamka tu."* (Sunan Darmi)

Hivyo basi ni lazima tuzingatia shabaha na kusudio hasa la kufunga saumu kila siku kisha tujiepushe na yale yote yaliokatazwa kuyafanya ndani ya saumu kama alivyotuelezea Mtume Mtukufu mwenyewe[saw] kwamba; *asiyeachana na kusema uwongo na kuufuata na ujinga basi, Allah Hana haja naye wala kujizuia kula na kunywa.* (Bukhari na Abu Dawood na matini yake ni ya Abu Dawood)

Kisha Mtume[saw] alisema katika hadithi nyingine kuwa; *"Atakayefunga saumu siku yoyote basi asiingiliane wala asitukane ama kuongea upuuzi. Na kama mtu mwingine amtukane na kutaka kupigana naye basi aseme mimi nimefunga saumu"* (Sahihul Bukhari na Muslim)

Mfunga saumu anatakiwa kudhibiti hisia zake, jazba yake na matamanio yake yote na kujitolea mno kwa kuacha vyakula vyake vipendezeshayo na ladha zake zote. Anajisikia kiu na maji yanakuwepo mbele yake lakini hayagusi kwa muda maalum, nafsi yake inamhumiza kwa kuvitumia vitu ila yeye hujizuia kwa ajili ya amri ya

Inaendelea uk. 5

Shabaha na Kusudio la Ramadhani

Kutoka uk. 4

Allah lakini hata hivyo kama kuna mtu ambaye haachi kusema uwongo na matendo ya kuwadanganya wengine au kuendelea na maradhi mbali mbali ya kiroho na kufanya maovu basi Allah hana haja ya kufunga kwake na saumu yake ni ya bure tu. Saumu ni kinga ya kumzuia Mtu kufanya matendo mabaya yote yaliyokatazwa na Allah Mtukufu na ni sababu ya kuisafisha na kuitakasa nafsi ya mfunga saumu, na kama yeyote hawezi kufaulu katika kupata shabaha hasa ya kufunga saumu basi kujizuia kwake kula na kunywa ni taabu ya bure tu.

Uwongo umetajwa hasa kwa sababu ni mama ya maradhi yote ya kiroho na kuna mtu anayeweza kujidhibiti nafsi yake na kujiepusha kabisa na kusema uwongo basi huyu mtu anaweza kuachana na maovu ya kila namna jinsi alivyoeleza Mtume[saw] kwenye hadithi yake na kumwambia yule bwana aliyemjia kwake ilhali alikuwa amezama katika maasi mengi na kujieleza kwamba anataka kujirekebisha n.k. hivo Mtume[saw] alimwambia kuwa aache kusema Uwongo naye aliahidi kwamba hatasema uwongo tena, na kwa ajili ya baraka ya kuacha uwongo aliweza kuachana na maovu ya kila namna.

Hazrat Mirza Nasir Ahmad[ra] Khalifa wa Tatu wa seyyedna Ahmad[as]. Anasema; *"Mwezi wa Ramadhani unakaribia kuja kwa baraka zake zote na sisi tunapaswa kujifaidisha kwa wingi kuipitia neema hii ya Allah Mtukufu. Tumeelekezwa kufanaya ibada za namna mbali mbali ndani ya mwezi huu. Imeelezwa sana juu ya kutoa haki za waja wa Mungu na kuhusu haki Zake Mungu. Mwezi wa Ramadhani umejikusanya ibada za namna tano.*

1. *Ya kwanza ni Saumu.*
2. *Ya pili imehimzwa kusimamisha sala kisha ni kusimama usiku yaani kusali nafali ya Tahajjud.*
3. *Ya tatu ni kusoma Qurani Kwa wingi.*
4. *Ya nne ni Ukarimu (kujitolea kwa mali na vipaji vyake vyote).*
5. *Ya tano ni kujilinda na maradhi (ya kiroho) ya nafsi,*

Mjumuiko wa ibada hizi tano za msingi unaitwa ibada za mwezi wa Ramadhani." (Khutbate Nasir, J.2.UK.954)

Ramadhani na Ukarimu

"Na mfano wa wale wanaotoa mali zao kwa kuitafuta radhi ya Allah na kujiimarisha wenyewe ni kama mfano wa bustani iliyo mahali pa juu, ikaifikia mvua kubwa na ikaleta matunda yake mara mbili na kama haifikiwi na mvua kubwa basi mvua ndogo (huitoshea) na Allah Anayaona mnayoyatenda." (Sura 2 Aya 266)

Mtume mtukufu[saw] alikuwa wa mwanzo katika kuonesha mfano uliotukuka mno wa kujitolea katika njia ya Allah na hivyo akazalisha mapinduzi hayo ndani ya wafuasi wake kwa kiwango cha kuishangaza dunia. Maisha yake yote yalijaa mifano ya kutoa mali katika njia ya Allah. Watu waliokuwa wanaishi karibu naye wanatuelezea ushuhuda wao wa dhati juu ya tabia tukufu ya bwana wetu Mtume[saw] kuwa yeye hakuwahi kumkataa mwombaji yeyote wala hakumrudisha yeyote kwa mikono mitupu aliyekuja kwake kuomba msaada.

Imesimuliwa na Hazrat Anas[ra] kwamba, *Mjumbe wa Allah[saw] hakuombwa chochote kwa jina la Islam isipokuwa akakitoa hicho.* (Muslim Kitabul Fadhail…)

Watu hata wasio waislamu walikuwa wanasema kumhusu Mtume[saw] kuwa *Muhammad anatoa kama anavyotoa yule asiyeogopa umaskini.* (Musnad Ahmad J.3.)

Allah amebainisha baraka za kutoa katika hadithi Qudsi pia kwamba, *"Ewe mwanadam! toa mali nitatoa kwa ajili yako."*

Hazrat Abdulla bin Amri[ra] anasima kuwa, Mtume[saw] alisema: *tunaweza kuona wivu kwa watu wa namna mbili tu. Mmoja ni yule Aliyejaaliwa neema ya Qurani naye anaisoma katika nyakati za usiku na wapili ni yule Aliyempa Allah mali nyingi naye anaitoa usiku na mchana katika njia ya Allah Mtukufu.* (Bukhari kitab Fadhailul Qurani)

Allah Alimjaalia Seyyidina Ahmad[as] Jumuiya ya watu wenye ikhlasi ambao walimsikia na wakamtii na wakaonyesha mifano mizuri ya kujitolea mali kwa ajili ya ustawi wa dini tukufu ya Kiislam. Hadhrat Masihe Mau`d (a.s) akieleza kuhusu kujitolea kwao alisema *"Idadi kubwa ya Jumuiya yangu ni maskini lakini namshukuru Allah kuwa ingawaje hii ni Jumuiya ya watu maskini lakini naona wana ukweli na huruma, wala hawasiti kutoa sawa na uwezo wao katika njia ya Allah baada ya kutambua mahitaji ya dini ya Islam"*.

Hazrat Babu Faqir Ali[ra]. alikuwa sahaba wa hazrat Masihe Maud as.ila alikuwa maskini. Siku moja katibu wa fedha alifika nyumbani kwake na kumwomba atoe chochote katika njia ya Allah. Babu Faqir Ali sahib alikuwa hana chochote nyumbani kwake zaidi ya kilo moja au nusu kilo ya unga wa kupikia usiku huu, hata hivyo aliingia ndani na kuchukua unga ule na kumpatia katibu wa fedha, halafu yeye na watoto wake walilala na njaa usiku ule.

Je, kuna mtaalamu yeyote wa dini nyingine yoyote anayeweza kutuletea mfano wa namna hii ya kujitolea katika njia ya Allah? Je, Allah alimuacha bila malipo hata katika dunia hii? Hapana, Wallahi alijaaliwa mtoto aliyekuwa nyota inga'ayo wa mbingu ya ki Ahmadiyya, aliyejulikana kwa jina la Maulana Naziir Ahmad Ally, Mbashiri wa kwanza wa Afrika Magharibi, aliyekuwa walii wa silisila hii ya Ahmadiyya.

Tukio hili lina somo hasa kwa ajili ya wale wanoasita sita kutoa mali, kwa kweli hawa wanamfuata shetani anayewaogofisha kupata ufukara, jinsi Asemavyo Allah, *"Shetani anawahofieni ufukara na kuamuruni kufanya ubaya. ilhali Allah anawaahidi msamaha wa madhambi na kupata Fadhili zake (kwa kutoa mali katika njia yake.)"*

Hivyobasitunapaswakujichunguza vizuri na kumuomba sana Mola wetu Mkarimu ili Atuwezeshe kutekeleza barabara wajibu wetu ulio juu yetu kuhusu mwezi huu mtukufu wa Ramadhani. Aamina.

Ramadhani na Qur'an



Kutoka uk. 1

zinamuombea mja, saumu itaomba hivi kuwa, E Mola wangu! Mimi nimemzuia kula na matamanio mengine mchana kutwa basi upokee maombezi yangu juu yake, na Qurani itasema, mimi nimemzuia kulala usiku (yaani aliendelea kusoma Qurani) basi ukubali maombezi yangu kumhusu yeye, basi maombezi yao (ya Quran na ya saumu) yatapokelewa." (Al-Baihaqi na Mishkat Kitab us Saum)

Kusoma Qurani Tukufu ndani ya Ramadhani tena kwa wingi asubuhi na jioni, mchana na usiku kwa mapenzi maalum ndio ibada muhimu ya Ramadhani.

Hazrat Abdulla bin Amri[ra] anasima kuwa, Mtume[saw] alisema: *tunaweza kuona wivu kwa watu wa namna mbili tu. Mmoja ni yule Aliyejaaliwa neema ya Qur'an naye anaisoma katika nyakati za usiku (na mchana) na wapili ni yule Aliyempa Allah mali nyingi naye anaitoa usiku na mchana katika njia ya Allah Mtukufu.* (Bukhari kitab Fadhailul Qurani)

Hazrat Ibne Abbas[ra] anasimulia kuwa, *Mjumbe wa Allah[saw] alikuwa mkarimu kuliko watu wote, alikuwa mkarimu zaidi mno katika Ramadhani ambapo Malaika Jibrili alikuwa anakutana naye. Na Jibrili alikuwa akikutana naye kila usiku katika mwezi wa Ramadhani na kusomeana naye Qurani Tukufu basi Mtume[saw] alipokuwa akikutana na Jibrili alikuwa anazidi sana katika ukarimu na wema kuliko upepo uvumao kasi.* (Bukhari kitab Badaul khalk)

Masood[ra] anasimulia kuwa Mjube wa Allah[saw] alisema: *Anayesoma herufi moja kutoka Qurani, atalipwa thawabu ya wema moja na kila wema unalipwa thawabu mara kumi. Sisemi kuwa: **Alif Laam Mim** ni herufi moja bali **Alif** ni herufi moja, **lam** ni herufi moja na **mim** ni herufi moja.* (Tirmazi Abwab Fadhailul Quran)

Kisha anasema Khalifa wetu kwamba: *Allah Ametufundisha njia ambazo kwazo tunaweza kupata Ukaribu naye na hudhihirika ishara za kupokelewa kwa maombi. Basi kukisoma kitabu hiki pia ni muhimmu sana. Kukisoma (kwa sauti nzuri) ni muhimu sana ndani ya Ramadhani, ili muelekeo wenu ukae huko mwaka mzima. Malaika Jibrili alimsomea Mtume[saw] Qurani mara mbili katika Ramadhani yake ya mwisho. (Bukhari kitab Fadhailul Quran). Hivyo basi mwaminio pia anatakiwa kujitahidi kuisoma Qurani yote mara mbili katika Ramadhani akifuata sunna hii (ya Mtume[saw]). Kama hawawezi kusoma (Qurani yote) mara mbili basi wasome angalau mara moja."* (Khutbate Masroor J.7.UK.413)

Kisha alisema Mtume[saw] akieleza muda wa kumaliza usomaji wa Qurani yote kuwa: *"Yule aliyesoma Qurani nzima katika muda wa siku chache kuliko tatu, yeye mtu huyu hakuielewa kitu (yaani Qurani isome taratibu kwa kuzingatia maana zake)."*

Ndio maana tunasema kuwa hairuhusiwi bali ni haifai kabisa kuisoma Qurani yote kabla ya siku tatu.

Seyyedna Hazrat Aqdas Masihe Maud[as] anasema: *"Hivyo chukueni tahadhari na msiende hata hatua moja kinyume na mafundisho ya Mungu na mwongozo wa Qurani Tukufu. Mimi nakuambieni kwa ukweli kabisa mtu hata akiepuka amri moja tu ndogo kati ya amri mia saba za Qurani ,huyu hujifungia kwa mkono wake mlango wa wokovu. Njia za kweli na kamilifu za wokovu imezifungua Qurani,na vingine vyote vilikuwa ni kama vivuli vyake. Kwa hiyo, someni Qurani kwa kuitafakari na muipende sana, kupenda ambako hamjakipenda chochote, sababu ni kama Alivyoniambia Allah: Heri zote zimo ndani ya Qurani tu. Na haya ndiyo kweli. Ole kwa wale watu, wanaotanguliza juu yake vitu vingine! Hakika Qurani Tukufu ni chemchem ya kufaulu kwenu, wokovu wenu wote. Hapana haja yoyote katika haja za dini zenu ila mtaipata katika Qurani Tukufu."* (Safina ya Nuhu uk.36.37 chapa cha 2018)

Bustani ya Washairi

RAMADHANI

1. Salamu ya Ramadhani, funga toka kwa Manani
Una siku Thelathini, kukuza zetu Imani

2. Karibu e Ramadhani, hapa kwetu duniani
Tunakualika nyumbani, waja tu viumbe duni

3. Twashukuru Ramadhani, kumfungia shetani
Fursa ilo bayani, kurudi kwa Rahmani

4. Ewe mwezi Ramadhani, Hatutangoja mwakani
Leo twasubiri nini, swaumu imo moyoni

5. Tufungeni Ramadhani, waja wote kwa makini
Mola aona riani, Adhabu yake Motoni.

Zaid A. Machombe (Mdogo)

ELIMU

1. Jifunze ilmu utavuna, maarifa na hekima aali
Elmu ina utukufu na dhima, hurahisisha kilicho ghali
Gumu likawa layina, utaheshimiwa watu watakujali

2. Kila mmuujiza uliofichikana, utatambua yake siri
Japo ndoto za mchana, utafahamu yake taa'wili
Akili yako itazindukana, magumu yakawa sahili

3. Zito likawa jepesi, wapata nguvu ya kusubiri
Mambo huwa mepesi, ukaweza mbali kusafiri
Ekaepukana na mikosi, yenye kudhoofisha mwili

4. Vitabu visome sana, mazito waweza badili
Akili yataka kusana, ndipo mengi utafidi
Utashirikiana na waungwana, wenye heshima na asili

5. Hofu yako itazama, nafsi yako itanawiri
Mola umkumbuke sana, usimuondoe katika akili
Ya leo sio ya jana, jifunze ilmu thaqili

6. Utaishi kwa mapana, utaondosha wako mushkili
Soma usiku na mchana, Mola atakujalia taufiki
Soma uzeeni na ujana, ujinga una madhili

7. Hakika ilmu itakulinda, na yako rasilimali
Utaepukana na inda, hutakuwa na dosari
Mola atakupenda, atakuondoshea kila hatari

8. Elmu nuru ing'aayo sana, huondosha giza likahama
Elmu chombo cha maana, usiwache nayo kushikamana
Japo umbali wa china, kaitafute siogope gharama

9. Elmu mbili zijue sana, ya dini na kimwili
Ala kuli hali, soma usifanye ubahili
Itakuondokea idhilali, moyo wako utanawiri

10. Soma kwa bidii, kila jambo kustahimili
Uvivu utupe mbali, utakuwa mtu kamili
Hakika ilmu ni mali, mali yataka tadbiri

11. Elimu ni nuru, kisha yataka maadili
Ikae katika suduru, Kisha yaongeza akili
Mola umshukuru, usome dua kwa takariri

12. Elmu ni bahari, weka mpango kamili
Mola Qahari, nia yako usibadili
Usifanye ufahari, usishike hili na hili

13. Weka mpango kamili, elimu uikabili
Elimu ni bahari, japo ile ya upili
Uwe mtu mahiri, usisahau jambo hili

14. Elimu huua ujinga, ikampandisha mja dhalili
Kisha hua kinga, humtoa mtu ujahili
Wendapo utaringa, soma upate nawiri

15. Utakapo utukufu na heshima, soma ilmu ikikubali
Ukweli na ubora wa kusema, na vitendo vyenye adili
Ukitaka umaarufu bila msingi, umetamania nafsi muhali

16. Kama nakshi jiweni, elimu uchangani
Sawa nakshi vumbini, elimu ukubwani
Elimu bora duniani, kumcha Mola manani

17. Mkamate sana elimu, usimwache aende zake
Kwa kila mbinu, mshike asikuponyoke
Ameletewa mwanadamu, kwa ajili ya uzima wake

18. Tamati Nabii kumsalia, na Ahli zake jamia
Sala na salaam kumfikia, na sahaba zake wasifiwa
Mola atupe afia, atuondoshee kila udhia

Al Haaj Abdallah S. Seif Al – Habsi
(Ben Habsi)

KIZAZI_TEULE

Ni kizazi teule, Kijukuu cha sahaba
Kilo vikwa usukule, Kwacha ya dini mahaba
Kilo sahau ya kale, Kumbu ni visa nasaba
Siye warithi wa Yule, Masihi muahidiwa

Neema nyingi hulevya, Hula nguvu ya maombi
Rohoni Uja huavya, Kumfanya mja zombi
Salani huanza chovya, ndipo hugeuka pimbi
Zisitulevye laghui, Na anasa za dunia

Shunda Mshudia wana
Daluni, Tanga

RAMADHANI UWE SABABU

1. Kama sifa za manani, mola Wa kushuriwa,
Alotupa Ramadhani, tupate kubarikiwa,
Kamtia kifungoni, shetani mlaaniwa,
Ramadhani we sababu, ya Allah kuniridhia.

2. Sababu we Ramadhani, nipate kurehemewa,
Neema za maishani, pate kumiminiwa,
Kumi kwanza Ramadhani, sipite me barikiwa,
Ramadhani we sababu, ya Allah kuniridhia.

3. Sababu we ramadhani, nipate kughofiriwa,
Madhambi ya maishani, nipate kusamehewa,
Kumi Pili ramadhani, si niache ni mtawa,
Ramadhani we sababu, ya Allah kuniridhia

4. Sababu we ramadhani, jahanamu okolewa,
Yaa tawwab niafuni, motoni kutounguwa,
Kumi mwisho ramadhani, moto kwangu ondolewa,
Ramadhani we sababu, ya Allah kuniridhia.

5. Tamati yaa ramadhani, si niache ni mkiwa,
Tahajudi qur-ani, nidumu bila pitiwa,
Rabbi yaa mu'uminun, imani sijepunguwa,
Ramadhani we sababu, ya Allah kuniridhia.

Masihi Omary Kisagwa

PENGO KAMA PENGO.

Kifo chaleta huzuni, kwandugu na marafiki,
Haijulikani lini, wala hakitabiliki,
Ajuae ni manani, yeye ndie mmiliki,
Pengo umetuachia, Hakuna wa kuziba.

Yatililika machozi, pale nikifikiria,
Safari hii ni njozi, leo umetangulia,
Tumeumbwa jozi jozi, na sisi tutafatia,
Pengo umetuachia, Hakuna wa kuziba.

Ulionyesha dhamira, waqfu ulijitoa,
Haukuwa na hasira, ukaikacha dunia,
Mola awape subira, jamaa na familia,
Pengo umetuachia, Hakuna wa kuziba.

Saliana Ramadhani Higiro

KUR-ANI NDIYO NJIA

1. Ukweli nimebaini, Kuraani muongozo,
Uloletwa duniani, Kutufunza makatazo,
Yatufikisha mbinguni, Tukishika maagizo,
Kuraani ndiyo njia, Yakutufika mbinguni.

2. Mtume ni Nabi wetu, Alotumwa na manani,
Kapewa kitabu chetu, Muongozo duniani,
Tusije kiacha katu, Chatuongoza duniani,
Kuraani ndiyo njia, Yakutufika mbinguni.

3. Mwenyezi kamteuwa, Kukamilisha imani,
Na elimu kupatiwa, Nayo ndiyo kuraani,
Naulinzi akapewa, Kuilinda kuraani,
Kuraani ndiyo njia, Yakutufika mbinguni.

4. Ni muongozo wa kweli, Wakutujenga imani,
Alotumwa ni mkweli, Kasifiwa duniani,
Mtume huyu mkweli, Hakika twamuamini,
Kuraani ndiyo njia, Yakutufika mbinguni.

5. Kitabu hiki chapeke, Sifa yake ni cha haki,
Elimu yake yap eke, Ni muongozo wa haki,
Hii ndiy'o sifa yake, Kutufunza yalo haki,
Kuraani ndiyo njia, Yakutufika mbinguni.

6. Chatuongoza imani, Mtume aliyesema,
Tukifateni jamani, Tuupate mwisho mwema,
Ndugu zanguni jamani, tukiheshimuni jamani,
Kuraani ndiyo njia, Yakutufika mbinguni

Madumla Ng'amilo

RAMADHAN KARIIM

Bodi ya Uhariri inawatakia wasomaji wetu wote wa gazeti hili heri ya mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Allah Atupe kila baraka kupitia mwezi huu.



Mfalme na Mawaziri Watatu

Hapo mwanzoni palikuwa na mfalme mmoja aliyewaita mawaziri wake watatu muhimu sana na akawapa kila mmoja wao mfuko. Aliwaambia waende huku na huko na kujaza mifuko aliyowapa kwa matunda. Huu ulikuwa ni mtihani wa uaminifu na ukweli wa mawaziri wake.

Waziri wa kwanza akaichukulia amri ya Mfalme kwa heshima na adabu sana na akakusanya kwa bidii matunda bora aliyoweza kuyapata na akajaza mfuko wake.



Waziri wa pili akaichukulia amri ya mfalme kiurahisi na akajaza mfuko wake kwa mchanganyiko wa matunda mazuri na mabovu.

Waziri wa tatu akafanya kinyume kabisa na mawaziri wenzake wawili. Aliujaza mfuko kwa majani makavu tu na uchafu. Nia yake ilikuwa ni kumpumbaza Mfalme kwa kumuonyesha tu kwamba ameshafanya kazi yake ya kujaza mfuko. Hakuwa na hata tunda moja katika mfuko wake.

Mawaziri wote watatuwakarejea kwenye baraza la mfalme na mifuko yao. Bila ya kuuliza nini walichokusanya, Mfalme akaamuru kila waziri kupelekwa katika jela tofauti kwa muda wa miezi mitatu. Chakula watakachokuwa wakila ni kile ambacho kila mmoja amejikusanyia katika mifuko yao.



Waziri wa kwanza alikuwa na furaha tu kwani alikuwa na chakula bora cha kutosha kula kwa siku zile. Hakuwa na hofu kabisa hata kidogo.

Waziri wa pili alipatwa na hofu maana nusu ya chakula chake kilikuwa kimeoza na kisingemfikisha kwa muda wote wa kuwepo jela.

Waziri wa tatu aligubikwa na hofu ya hatari zaidi kwani hakuwa na chakula kabisa. Alipuuzia na kufanya uzembe katika kutekeleza amri ya Mfalme.

• • • •

Ramadhani na Ibada

Kusudio hasa la kuumbwa kwa binadamu ni kumuabudu Allah Subhanahu wa Taalah. Allah Amesema ndani ya Qurani Tukufu: *Na sikuwaumba majinni na watu ila wapate kuniabudu mimi.* (51:57)

Kisha Allah Anasema Akieleza sifa za waaminio kwamba: *Huinuka mabavu zao kutoka vitandani kumuomba Mola wao, kwa hofu na tumaini.*(As-Sajda:17)

Bwana wetu Mtume Mtukufu[saw] alisema; *Kwa yakini kila kitu kinakuwa na mlango wake na mlango wa ibada ni saumu.*(Al-Jame'e Asaghiir)

Nasaha hii ya bwana wetu Mtukuf[saw] ni yenye hekima na busara sana kwamba mlango wa ibada ni saumu na kama mnataka kuingia kwenye ukulu wa ibada basi mtaingia humo kupitia saumu kwa sababu saumu zinamzuia mtu na maovu ya kila namna. Mfunga saumu anajizuia kusema uwongo, kusengeneya, kushiriki katika mikutano ya muziki, kushutumiana, kulaumiana, kugombana n.k. na maibu yake yananza kuondoka kwake na pamoja na haya anaanza kusogea kwenye wema wa kila namna na jinsi anavyopata kujitakasa na kujisafisha kupitia saumu basi sala zake zinapata kuhuika na kuboreka na anaanza kupata jazba na ladha katika kutekeleza wajibu wake ulio juu yake kutokana na kumuabudu Allah Mtukufu basi sala tano ni kipimo cha kujua usafi na utakaso wa ndani mwetu na kueleza uhusiano wetu na ukaribu na Allah Mtukufu. Kama tunazingatia sala tano kila siku basi pole pole tutaanza kupata ladha na raha humo na kupata utulivu kwa kuingia msikitini na jinsi tutaendelea kupata utakaso na usafi wa mioyo hivyo tutaendelea kupata ladha na utulivu kwenye ibada zetu na kuzidi katika kumpenda Allah kisha tutazidi katika kusali si sala za faradhi tu bali kwenye sala za nafli pia yaani Tahajjud.

Khalifa wetu wa Tano hazrat Mirza Masroor Ahmad[atba] anasema: *Imesimuliwa kwenye hadithi moja kuwa kiini cha ibada ndio sala. Basi muaminio anapaswa kuwa na lengo la kupata kiini hiki…*(Khutbate Masroor J.6.UK.164)

Hali ya kumkumbuka Allah kwa wingi inatakiwa ipatikane angalau katika siku tukufu za Ramadhani kwa uchache na tutafute muda wa kukaa faraghani kwa ajili ya kumkumbuka Allah, kusoma Tasbiih, kuomba dua mbali mbali, kusoma Qurani na Kusali sala ya nafli ili tupate baraka nyingi zaidi za Ramadhani.

Tahajjudi (sala ya usiku)

Sala ya Tahajjud ni sala inayosaliwa katika sehemu ya mwisho wa usiku kabla ya mapambazuko ya Alfajiri na sala hiyo si faradhi lakini ina baraka nyingi zaidi na ni sunna ya watu wema wote kusali sala hiyo kila siku. Imesisitizwa ndani ya Qurani Tukufu juu ya kusali sala ya Tahajjud. Allah Anasema akieleza umuhimmu na baraka za sala ya Tahajuud kwamba:

"*na katika usiku pia amka na kusali Tahajjud kwa (kuisoma Qurani) ndio (ibada) zaidi kwako. Huenda Mola Wako Akakuinua cheo kinachosifika.*"
(Sura Bani Israeli, 17:80)

Kisha Anasema Mungu Mwenye Enzi Akieleza tabia ya waaminio kuwa: -"*Huinuka mbavu zao kutoka vitandani kumwomba Mola wao kwa hofu na tumaini.*" (Al-Quran 32:17)

Anasema pengine Mungu Mtukufu kuhusu sifa za watu wema kwamba: -"*Walikuwa wakilala kidogo tu usiku.*" (Al-Quran 51:18)

Imesimuliwa na Hazrat Abu Hurairah[ra] ya kwamba Mtume[saw] alisema, *ifikapo sehemu ya mwisho ya usiku basi Mola wetu Huteremka katika mbingu ya karibu kila siku na Husema: kuna yeyote wa kuniomba dua, Nami nimkubalie dua yake? Kuna yeyote wa kuniomba ghofira, Nami nimghofirie? Kuna yeyote wa kuniomba riziki, Nami nimpatie riziki? Kuna yeyote wa kuniomba dua ya kumuondolea shida yake, Nami nimuondolee shida yake? Allah huendelea kusema hiyo hadi kupambazuka.*" (Musnad Ahmad bin Hambali J.2.UK.521.chapa ya Beiruti)

Wenye shida na taabu wanatakiwa kujaribu kutumia njia hii ya kuondoa shida na taabu zao.



Hazrat Aqdas Masihe Maud[as] anasema: *"watu wamedhani kuwa "nafil" (ibada ya hiyari) ni zile tu zinazosaliwa na sala. Hapana sio hivyo. Nawafil ziko pamoja na kila kitendo. Mtu anapotoa Zaka basi atoe(zaidi) pia psipo Zaka. Anapofunga saumu ya Ramadhani basi afunge katika zingine pia. Anapokopa basi arudishe zaidi kiasi(pamoja na pesa zenyewe)….matokeo yako yanakuwa hivi kuwa Anasema (Mungu) kwamba Ninakuwa kama jicho la waaminio na wale waliopata ukaribu nami, yaani macho yao yanakaa pale tu ambapo Napapenda. ..Nakuwa masikio yao.. ni dokezo kwenye jambo hili kwamba popote pale Allah au Mtume wake au kitabu chake kinafanyiwa mzaha, wanaondoka na kutoka huko wakichukia na kukasirika, hawawezi kuyasikia na hawasikii neno lolote ambalo linakuwa kinyume cha ridha ya Allah na amri Yake na hawakai katika vikao vya namna hii hali kadhalika wanajiepusha na maneno ya ufasiki na ya uasi, na manzari mabaya ya (mahafali ya kusikiliza (muziki) na sauti (mbaya). Kupata mawazo mabaya kwa kusikia sauti ya yule aliyekatazwa kusikiliza sauti yake ni "Zinaa ul Uzun" (yaani uzinifu wa masikio)… kisha Anasema(Mungu) Ninakuwa mikono yake. Mtu hufanya kitendo cha kutokurehemu baadhi ya wakati. Allah Anasema mikono ya muaminio hayaruki kwenye uadilifu bila sababu. Hawagusi wale waliokatazwa kuwagusa. Kisha Anasema, Ninakuwa ulimi wake, (wala hasemi kwa tamaa ya nafsi yake:* sura Al-Najm aya:4*) Inadokeza kwenye hili. Hivyo yale aliyoyasema Mtume wa Allah[saw] yalikuwa ya Allah. Na kwa ajili ya mkono wake (Mtume[saw]) Alisema: Kwa kifupi, mtu hupta daraja la juu kabisa na ukaribu kwa (kusali) nafli hadi anaingia kwenye kundi la wapenzi (mawalii) wa Allaha Mtukufu.*"(Malfuzat J.1.UK.437-438)

Mtume wetu Mtukufu[saw] alikuwa anasali sala ndefu ndefu wakati wa usiku na bi Aaisha[ra] alipoulizwa kuhusu sala yake ya usiku (sala ya Tahajjud) alisema: *Mtume[saw] alikuwa anasali rakaa 11 katika mwezi wa Ramadhani au katika siku zingine pia. Wala usiniulize juu ya uzuri na urefu wake yaani alikuwa anarefusha sana kisha alikuwa anasali kwa uzuri mno na sina maneno yaelezayo ubora wa sala yake ya usiku.* (Bukhari Kitabul Jumaa)

Hazrat Masihe Maud[as] anasema: *"Jamaati yetu inatakiwa wajilazimishe kusali sala ya Tahajjud. Yule asiyeweza kusali zaidi basi angalau asali rakaa mbili, kwa sababu, kwa hali yoyote ile, atapata nafasi ya kuomba dua. Dua za wakati huo zina athari maalum kwani hutoka kwa uchungu na jazba ya kweli."*(Malfoozat J.2.UK.182)

Hazrat Khalifatul Masih wa nne[rh] anasema: *Jambo moja ambalo nimeshuhudia katika Qadian, kuhusu saumu ya Ramadhani…nalo ni hili kwamba (wazazi) walikuwa hawaamshi Watoto wao katika muda ambao ulikuwa unatosha kwa ajili ya kula daku tu, bali lazima walikuwa wanawaamsha mapema kwa wakati uliokuwa unafaa kwa ajili ya kusali rakaa 2 au nne hivi kwa uchache na mama zao walikuwa hawawapi daku hadi kumaliza nafali. Kwanza kabisa walikuwa wanaandalia udhuu kisha kusali ili wapate kujua kuwa lengo hasa la saumu ni kujifunza maisha ya kiroho. Wasali* ***Tahajjud****, wasome* ***Qurani Tukufu*** *kisha waaje kula daku pia.* (khutba ya Ijumaa, 30 May 1986)

Huzur, Hazrat Mirza Tahir Ahmad[rh]. anasema pengine: *"Asiwepo Muahmadiyya hata mmoja dunia (kote) asiyezoea kusali sala ya* ***Tahajjud ndani ya Ramdhani Kareem****…kwa hakika kula daku katika Ramadhani si Ramadhani iyenewe bali kula chakula cha kiroho kabla ya kula daku yaani kusali nafali ndio Ramadhani hasa.*" (Khutbate Tahir J.8.UK.225)

Hazrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifa wetu wa Tano ATBA anasema: *Allah Atujaalie kufanya maombi ndani ya Ramadhani hii kama wapenzi wake…Allah Mtukufu Atuwezeshe kuwa waja wake wanaomuabudu kikweli..Allah Mtukufu Aturehemu, Atujalie fadhila zake na Atuoneshe ushindi wa Ahmadiyya yaani ya dini ya kweli katika Maisha yetu na siku za ushindi wetu juu ya dunia nzima. Ewe Mwenyezi! Utujaalie sehemu ya baraka za Ramadhani isiyohesabika, Atulinde na kila shari na Aendelee kutufunika na shuka la rehema na fadhila zake daima dwamu. Aamina.*
(Khutbate Masroor J.1.UK.433-48)

Sala ya Tarawehe

Sala ya Tarawehe kwa kweli ni sala ya Tahajjud. Imeruhusiwa kusali mwanzoni mwa usiku yaani baada ya sala ya Ishaa ndani ya mwezi wa Ramadhani kwa watu wa kwaida ili wajifaidishe nayo. Sala hii imeenea zaidi katika enzi za ukhalifa wa hazrat Omar[ra]. Ni bora zaidi kama sala hii inasaliwa katika sehemu ya mwisho wa usiku hata ndani ya Ramadhani. Sala hii inasaliwa rakaa nane ila kama mtu yeyote akitaka kuongeza idadi ya rakaa na kusali rakaa 20 pia inajuzu na kupumzika kidogo baada ya kumaliza kila rakaa 4 inapendeza. Sala ya Taraweh inasaliwa rakaa mbili mbili.

Hazrat Masihe Maud[as] aliwahi kusema safari moja kwamba: *Kusali rakaa nane ni sunna ya Mtume[saw] iliyodumu naye alikuwa anasali wakati wa Tahajjud (yaani katika sehemu ya mwisho ya usiku) na hii ndio bora zaidi lakini inajuzu pia kusali katika sehemu ya mwanzo mwa usiku. Imeandikwa katika riwaya moja kwamba Yeye (saw) aliisali katika sehemu ya mwanzo mwa usiku. Rakaa 20 zilisaliwa baadaye.*
(Fatawa ya Mashie Maud[as] UK.71)

Ikumbukwe kuwa kama mtu yeyote anasali rakaa 20 basi ni hiyari yake mwenyewe. Kuna riwaya inayoeleza kwamba Taraweh imesaliwa rakaa 20 pia wakati wa Hazrat Omar[ra]. Lakini sawa na sunna ya Mtume[saw] iliyodumu zaidi ni rakaa 8 tu naye[saw] alikuwa anasali wakati wa Tahajjud.

Imesimuliwa na Hazrat Abu Salmah bin Abdur Rehmani kwamba yeye alimuuliza bi Aaisha[ra] kuwa: *ilikuwaje sala ya usiku ya Mtume[saw]? Yeye[ra]. Alijibu! Mtume[saw] hakuwa akizidisha-si katika Ramadhani wala katika mwezi mwingine wowote-zaidi ya rakaa 11. Alikuwa akisali rakaa nne (na kupumzika kidogo) basi usiulize urefu na uzuri wake! kisha akisali rakaa nne, usiniulize urefu na uzuri wake! kisha akisali rakaa tatu (za Witri).* (Bukhari Kitab Salat ut Taraweh Bab Man Qama Ramadhana).

Riwaya hii inathibitisha kuwa kusali rakaa nane ya Tarawehe ni Sunna ya Mtume[saw] lakini kwa kuwa sala ya Taraweh ni sala ya nafali hivyo basi yeyote akitaka kuongeza rakaa zaidi ya 8, anaruhusiwa kwani watu walikuwa wamezoea kusali rakaa 20 katika nyakati za Hazrat Omar[ra], ili usomaji wa kila rakaa uiishi haraka na watu wasilazimike kusimama sana kwenye rakaa moja tu kwa sababu muda mwingine watu walikuwa wanachoka kutokana na usomaji mrefu (wa Qurani Tukufu katika kila rakaa kwani ni desturi ya kumaliza Qurani Tukufu jizu yote 30 kwa siku 30 hivi). (imechukuliwa kutoka Fiqha ya Ahmadiyya J.1.uk. 209)

Kwa kifupi kusali sala ya Tahajuud katika Ramadhani ni bora zaidi.

MASUALA YA KIFIQHI

Kufunga ni moja ya nguzo za msingi za Islam n ani lazima kuzitimiza pia. Kuna baadhi ya maswali madogo madogo yanayoulizwa kuhusu saumu, muda wa kula daku, muda wa kufuturu na hukumu ya kufunga mtu akiwa mgonjwa au safarini.

Tunao wajibu wa kuwapatia hawa wote majibu muafaka ya maswali hayo ili mioyoni mwao musibaki wasiwasi na wapate utulivu.

KUUONA MWEZI

Allah Anasema: "*Basi atakayeuona mwezi miongoni mwenu, afunge Saumu*."

Mtume Mtukufu^{saw} anasema: *Fungeni saumu kwa kuuona mwezi na kufuturu pia kwa kuuona mwezi na kumetanda kwenu basi timizeni siku za Shaabani kuwa thelathini*.

Imesimuliwa na Hazrat Ibne Omar^{ra} kuwa, Mtume^{saw} alisema: *msifunge saumu mpaka muione Hilal wala msifuturu mpaka muione (Hilal) na kama kumetanda kwenu basi muikadirie (Hilal).* (Sahih Muslim)

Yaani mutimize siku thelathini ya mwezi wa Shaabani. na wala msiache kufunga bila kuuona mwezi mpya.

Masihi Aliyeahidiwa^{as} amesema *daima tusifuate tu mahesabu au nadharia. Makosa yanaweza kutokea. Ni jambo la wazi kwamba mtu asitegemee moja kwa moja juu ya sayansi bali pia afuate kuonekana kwa mwezi mwandamo. Pia mtu azingatie kwamba siku za kufunga hazizidi 30*. Masihi Aliyeahidiwa^{as} amesema "*Kuuona mwezi ni jambo bora zaidi kuliko mahesabu. Baada ya kufanya uchunguzi wa kutosha juu ya hili, maulamaa wengi wa Ulaya wameonelea ni vyema kuushuhudia mwezi mwandamo*."

(kifupisho toka Khutba ya Ijumaa ya 03-06-2016)

Nia ya Saumu

"Hazrat Hafsa^{ra} anasema kuwa, Mtume^{saw} alisema: *hakuna Saumu kwa yule asiyefunga nia kabla ya Alfajiri*."

(Abu Dawood Kitabus Siyam Babu nia)

Nia ni matakwa ya moyo kwa hakika wala haihitaji maneno maalum kwamba mfunga saumu anafunga kwa ajili ya nani.

Ila mfunga saumu anaweza kuyasoma maneno yafuatayo.

"*Nimenuia kufunga saumu ya kesho ndani ya mwezi wa Ramadhani*."

Ikumbukwe kuwa dua hii haipatikani katika Hadithi yoyote na nia ni matakwa ya moyo au adhma ya mtu tu, iliyo muhimu zaidi lakini kama kuna mtu asiyeweza kuamka kabla ya mapambazuko ila alikuwa na nia ya kufunga Saumu basi anaruhusiwa kufunga bila ya kula daku na bila ya kufunga nia kabla ya mapambazuko.

Umuhimu wa Kula Daku

1. Imesimuliwa na Hazrat Anas^{ra} ya kwamba Mtume^{saw} alisema: *kuleni Daku, bila shaka kuna baraka katika kula daku*. (Bukhari kitabus Saum bab barakatus-suhuri)

Kuna baraka za namna mbili zinazopatikana katika kula daku. Baraka ya kwanza ni kula daku ambacho ni muhimu kwa ajili ya kukimu mgongo wake na kwa ajili ya kupata nguvu mwilini na baraka ya pili ni kuamka usiku na kupata muda wa kusali sala ya Tahajjud na kuomba maombi kwani maombi ya wakati ule yanaathari maalum na yanakubaliwa zaidi. kisha mfunga saumu anaweza kusali sala ya Alfajiri kwa urahisi na kusoma Qurani Tukufu na anaweza kupata baraka ya kutekeleza amri ya kusoma Qurani Alfajiri jinsi Alivyoamrisha Allah kuwa: "*Soma Qurani Alfajiri*."

Hazrat Mirza Bashiruddin sahib^{ra} alisema kwamba katika mwaka 1903, Dr Khalifa Rashid ud Din sahib na mkewe^{ra} walikuja Qadian na kubaki kwa siku nne. Wakaonyesha hamu yao ya kufunga wakiwa Qadian. Masihi Aliyeahidiwa^{as} akawaletea daku ya chapati za Kashmiri, na akawahudumia yeye mwenyewe. Kisha akasikia adhana na Masihi Aliyeahidiwa^{as} akawaambia Allah anasema katika Quran tukufu: "*Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu uzi mweupe kutoka katika uzi mweusi wa alfajiri*." (2:188)

Masihi Aliyeahidiwa^{as} akasema *watu hawafuati amri hii na hivyo kuwataka waendee kula wakati adhana inaendelea na pia akasema mwadhini siku hiyo aliadhini mapema.*

*Mtu anaweza kutumia chakula kizuri lakini kwa kiasi na mizania. Allah anasema katika Quran tukufu: "**Allah Huwatakieni yaliyo mepesi wala Hawatakieni yaliyo mazito.**"* (2:186) *Saumu imelazimishwa ili kuyarahisisha maisha ya mwaminio na kumwepusha na shida. Lakini baadhi ya watu wanaofikiria kwamba wanashinda na njaa mwezi wa Ramadhani, kwa hakika wanazitusi amri za Quran tukufu.*

Chakula hasa ni chakula cha kiroho, ambacho kinazirutubisha roho badala ya chakula cha kimwili kinachourutubisha mwili tu. Mtu anatakiwa ajitambue kwamba anafunga na hivyo ale kwa kiasi. Baadhi ya watu huishia kuongezeka uzito badala ya kupungua wakati wa Ramadhani. Kwa baadhi ya watu mawazo yote yanakuwa ni kujaza matumbo yao tu badala ya saumu. Wanajilia tu vyakula vya mafuta mengi na tamtam kupita kiasi.

Jambo hili hupunguza baraka za Ramadhan. Kuna amri ya kuwahi kufuutru na kula daku na hayo ndio yenye baraka. Mtu anatakiwa kula chakula kizuri lakini kwa kiasi.

(kutoka Hotuba ya Ijumaa ya 03-06-2016, Muhtasari wake)

Kuhusu wakati wa Kufuturu

Allah Anasema: "*Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu uzi mweupe katika uzi mweusi wa Alfajiri kisha timizeni Saumu mpaka usiku*." (A-baqarah 2: 188

1. Hazrat Omar bin Khattab anasimulia ya kuwa, Mtume^{saw} alisema: "*Usiku unapoingia tokea upande wa mashariki na mchana unapotoweka upande wa magharibi na jua linapotua, basi hapo afungae Saumu hana budi kufuturu*." (Bukhari na Muslim)

2. Hazrat Abdullah bin Abi Aufa^{ra} anasimulia ya kuwa tulisafiri pamoja na Mtume^{saw} hali yeye alikuwa amefunga Saumu ya nafli (ya hiyari), lilipotua jua alimwambia mmoja wetu "*shuka na utupikie ugali wa shayiri iliyosagwa", akamjibu: Ewe Mjumbe wa Mungu ungesubiri giza liingie. Mtume^{saw} akamuamuru shuka na utupikie ugali wa shayiri iliyosagwa. Akamjibu: Baado kungali mchana ewe. Mtume^{saw} akamuamuru mara ya tatu "shuka na ututayarishie ugali" Msimuliaji anasimulia: mtu huyu alishuka akawatayarishia ugali na Mtume^{saw} huku akila alionyesha upande wa mashariki na akawaambia: Mtakapoona giza linaingia upande wa mashariki basi afungae Saumu afuturu*." (Sahihul Bukhari na muslim)

3. Hazrat Abu Hurairah^{ra} anasimulia kuwa, Mtume^{saw} alisema: "*watu wataendelea katika heri madamu wanafuturu mapema. Futuruni mapema kwani Mayahudi wanachelewa kufututru*. (Ibne Majah Kitabus Saum….)

Vyakula Vipendezavyo katika Kufuturu

Hazrat Salman bin Aamir Dhabbi^{ra} anasimulia ya kuwa Mtume^{saw} alisema: "*Fungueni Saumu yenu kwa kula tende au kunywa maji yalio safi na mazuri*." (Sunana Abu Dawood)

Kuna hadithi zingine zinatoa maelezo zaidi kwamba kwa hakika mfunga Saumu anaweza kufuturu kwa kitu cho chote kinachopatikana kwa urahisi ilmuradi kiwe halali tu, kama tende, maji, chumvi au kwa kuchanganya maziwa kiasi(mafunda machache) katika maji na kadhalika.

Dua Inayosomwa Wakati wa Kufuturu

1. Hazrat Mu'az bin Zahrah^{ra} anasimulia kuwa, Mtume^{saw} alipokuwa akifuturu alikuwa anaomba kwa maneno yafuatayo:

"*Ewe Mola wangu, kwa ajili yako nilifunga na ninafuturu kwa riziki uliyonipa*." (Abu Dawood kitabus Siyam babul kaul indal iftar)

2. Hazrat Ibne Omar^{ra} anasimulia ya kuwa, Mtume^{saw} alipokuwa akifuturu alikuwa anasema: "*Kiu kimetoka, mishipa imelowa na ujira umethibitika, Mungu Akijalia*." (Abu Dawood kitabus Siyam babul kaul indal iftar)

Thawabu ya kufuturisha

1. Hazrat Zaid bin Khalid Al-Juhani^{ra} ya kwamba, Nabii^{saw} alisema: *Yule aliyemfuturisha mfunga Saumu atapata thawabu sawa na thawabu ya mwenye kufunga bila ya thawabu ya mfunga Saumu kupungua hata kidogo.* (Jame'e Tirmazi kitabus Saum)

Kuna watu ambao wana mawazo mabovu kabisa kwamba lazima tuwe na chakula kizuri cha aina Fulani kama mihogo, wali, tamtam n.k. lakini wanasahau kuwa Ramadhan inawafundisha adabu na kuvumilia juu ya kile kinachopatikana kwa urahisi bila kuwaletea shida na taabu watu wa nyumbani.

Kula Chakula Mbele ya Mfunga Saumu

Umme Ammarah^{ra} anasimulia ya kuwa, *Mtume^{saw} alimzuru naye akamuandalia chakula mbele yake. Mtume^{saw} alimwambia; Tule pamoja, alimjibu: Mimi nimefunga Saumu, Mtume^{saw} alimwambia: Malaika huwasalia wafungao Saumu madamu watu wanakula mbele yao mpaka watakapokwisha kula. Pengine alimwambia, wameshiba*" (Jame'e Tirmazi)

Hadithi hii inaeleza habari ya Saumu ya nafali lakini si maana yake kwamba thawabu na baraka hizi hazitapatikana kwa Saumu ya Ramadhani bali kwa kuwa Saumu ya Ramadhani ni faradhi basi thawabu na baraka hizi zitaongezeka maradufu, Akijalia Allah. Kisha hakuna marufuku kwa kula chakula mbele ya mfunga Saumu kama mwenye kula hajafunga wala hakuna dhambi juu yake.

Kisha inaelezwa pia kuwa kama mfunga Saumu amesahau na anaendelea kula basi mwenye kujua na kumwona asimkumbushie wala asimkataze kula au kunywa hadi mfunga Saumu mwenywe ajue na ajizuie kula au kunywa, kwani Mtume^{saw} alisema kuwa Mungu ndiye Aliyemlisha Mfunga Saumu na kama Mungu Anamlisha sisi ni nani wa kumzuia?

Saumu ya Mgonjwa na Msafiri

Mungu Mwenye Enzi Anasema: "*Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini basi atomize hesabu katika siku zingine*." (Suratul Baqarah 2:186)

1. Hazrat Anas bin Malik^{ra} anasimulia ya kwamba, *kuna mtu akaja kwa Mtume^{saw} (mjini) Madina, Yeye alikuwa anakula wakati wa mchana, yeye^{saw} alisema njoo ule chakula. Yule alijibu nimefunga Saumu. Yeye^{saw} alisema: kwa hakika Allah Ameshaondoa Saumu na nusu ya sala kwa msafiri, hali kadhalika Saumu zimeondolewa kwa mwanamke mwenye mimba au anayenyonyesha.* (Nasai kitabus Siyam)

2. Imesimuliwa na Hazrat Jabir bin Abdulla^{ra} kwamba yeye anasema, *Mtume^{saw} alikuwa safarini siku moja na aliona mkusanyiko wa watu na kumuona mtu aliyewekwa kivulini. Mtume^{saw} aliuliza kuna nini? Watu walijibu: kuna mfunga Saumu. Mtume^{saw} alisema: "**Si wema kufunga Saumu katika safari.**"*

3. Hazrat Ibne Abbas^{ra} anasimulia ya kwamba, *Mtume^{saw} alitoka Madina na kuelekea Makkah naye alikuwa amefunga Saumu hadi alipofika Asfaan basi aliagiza maji na akainua juu (kikombe cha maji) kwa mikono yake na kuwaonesha watu kisha akafuturu na kuingia Makka na haya yalitokea ndani ya Ramadhani.* (Bukhari kitabus Saum babu man aftara fis safari)

4. Hazrat Ibne Omar^{ra} anasimulia kuwa, Mtume^{saw} alisema:

"*Kwa hakika Allah Mtukufu Anapenda zitekelezwe ruhusa Alizotoa kama Anavyochukia Kutendwa maasi*." (Musnad Ahmad bin Hambal)

Hivyo basi lazima tujifaidishe na ruhusa zilizotolewa na Mungu wala hatuwezi kumridhisha kwa nguvu zetu. Mgonjwa na msafiri ameamrishwa kutimiza hesabu katika siku zingine.

Inaendelea uk. 10

Kutoka uk. 9

Kama vile Allah alivyoamrisha kufunga saumu, pia ameamrisha kutokufunga katika mazingira fulani.

Fidia Ya Saumu

Allah anasema: "*Na wale wasioiweza (kufunga Saumu) watoe fidia kwa kumlisha maskini.*" (Al-Baqarah 2:185)

Maneno haya yanaeleza habari za watu walio wazee sana, au wanawake wanaonyonyesha Watoto wao, au wenye mimba, au watu wasio na afya nzuri. Yaani wakifunga watajitaabisha na taabu isiyovumilika. Basi watu wa namna hii wasifunge bali watoe fidia kwa kumlisha maskini chakula sawa na chakula wanachotumia wenyewe kwa muda wa siku za Saumu.

Hazrat Ibne Abbas^{ra} anasema kuwa, maana ya neno "*Yutiqoonahu*" ni wasioweza. Wanapata shida sana na Saumu, yaani mtu ambaya ni mzee sana au mwanamke wasiyoweza kufunga basi wamlishe maskini mmoja juu ya kila Saumu. (Sahih ul Bukhari kitab ut Tafsir)

Seyyedna Hazrat Ahmad^{as} anasema: "*Allah Ameweka msingi wa sheria juu ya urahisi, msafiri au mgonjwa anayeweza basi watoe fidia na wasifunge Saumu. Fidia ni kumlisha maskini chakula……. (mradi wa mgonjwa au msafiri ni mtu ambaye hataraji kufunga tena mbele)….. kutoa fidia tu, inaweza kuwahusu wazee sana au wale tu wanaofanana nao, wasioweza kabisa kuwa na uwezo wa kwaida, waila mawazo ya kutoa fidia, kwa kwa ajili ya watu wa kwaida wanaoweza kufunga baadaye (baada ya kupata afya) ni sawa sawa na kuwaruhus tu moja kwa moja. Dini isiyokuwa na ijtihada haina thamani mbele yetu. Na kuondoa maagizo ya Mungu kwa njia hii ni dhmbai kubwa. Allah Ameshasema kuwa, wale wanaojitahidi katika njia yako ndio watakaoongozwa.*"
(Malfoozat J.5.UK.321-22)

Kiwango cha Fidia

Allah anasema akieleza kiwango cha Fidia kuwa: *sawa na kiwango mnachowalisha ahali zenu*.(Al-Baqara) Basi kiwango hiki kichukuliwe na kila mwaminio, Tajiri atoe sawa na wasa wake na maskini sawa na uwezo wake. Isipokuwa kama kuna mtu ambaye hawezi kutoa fidia basi afanye toba na aombe msamaha, ghofira na rehema kutoka kwa Allah na Yeye ndiye Anayejua siri zote na Anaweza kumsamehe.

Kisha si lazima kuwa, fidia ya Saumu za Ramadhan ipelekwe kwa mtu yule tu anayefunga Saumu au lazima awe Muislam kwani masharti haya hayakuelezwa na Allah, basi fidia ya saumu inaweza kumlipa maskini yeyote ila katika Jumuiyya yetu tuna taratibu zake za kuipokea na kuipeleka kwa watu husika hivyo tuitoe katika Jamaati.

Imama Abu Hunifa^{rh} amesema kiwango cha fidia ya siku moja ni sawa na nusu "*sa'a*" ya ngano yaani kilo mbili kasa robo ya ngano lakini watafiti wengine wamesema kuwa sa'a moja inazidi kidogo kuliko kilo mbili. (Fiqha Ahmadiyya J.1.UK.296)

Sawa na taratibu zetu za Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya, tunatangaziwa kila mwaka na Amiri na Mbashiri Mkuu wetu wa nchini kwa hiyo tunatakiwa kuufuata ule mwongozo kikamilifu.

Mambo Ambayo Hayaharibu Saumu

1. Kula na kunywa kwa kusahau:
Mtume^{saw} alisema: "*Atakayesahau naye amefunga, akala au akanywa basi atimize Saumu yake, kwani ni Allah ndiye Aliyemlisha na kumnyewisha.*" (Bukhari na Muslim)

2. Kutapika
Mtume^{saw} alisema: "*Atakayelemewa na matapishi, hapaswi kulipia (Saumu) na anayejitapisha inampasa kuilipia.*" (Muttafiq Alaihe).

Hivyo kama mtu yeyote anapata kutapika muda Fulani na haoni shida basi aendelee na saumu yake ila akiona taaba na kushindwa kutimiza saumu basi anaruhusiwa kufungua lakini ataitimiza katika siku nyingine.

3. Janaba
Bi Aaisha na Ummu Salma^{ra} wanasimulia kuwa, *Mtume^{saw} alikuwa akipambanukiwa akiwa na janaba la kujamii kisha akioga, na akiendelea na Saumu*."(Muttafiq Alaihe)

4. Mtume^{saw} alisema: "*mambo matatu hayaharibu Saumu, ambayo ni kukata nywele, kutapika na janaba*."(Tirmizi)

Nb: baadhi wakati vijana wanala baada ya kula Daku au mchana na kupata janaba kwa kuoteshwa kwa ndoto basi Saumu zao haziharibik wanatakiwa kuoga tu kwa haraka iwezekanavyo na kama kuna mtu aliyechelewa kuamka na ana muda wa kula daku au kuoga tu basi ale daku kisha aoge na aende kusali msikitini.lakini yule aliye chelewa zaidi na kuamka baada ya alfajiri na anaweza kufunga Saumu bila kula daku basi aweke nia ya Saumu na aendelee na Saumu isipokuwa nia ya saumu ni muhimu mapema kabla ya Adhuhuri.

Kama yeyote anaharibu Saumu yake mwenyewe basi adhabu yake ni kufunga siku 60 au kuwalisha chakula maskini 60.

5. Kupaka wanja
Mwanamke anaweza kupaka wanja wakati wa mchana ama mwanume, *Mtume^{saw} alisema: usipake wanja wakati wa mchana hali umefunga Saumu*".
(Musnad Darmi Babul Kahli)
Imam uz zaman Seyyedna Ahmad^{as} anasema: "*kuna haja gani ya kupaka wanja wakati wa mchana, Apake usiku*."(Al-Badri 3/1907 kupitia Fiqha ya Ahmadiyya)

6. Kuumika
Hazrat Abdullah bin Abbas^{ra} anasimulia ya kwamba, *Mtume^{saw} aliumika naye amefunga Ihramu. Na ameumika naye amefunga.* (Bukhari)

7. Kumbusu Mtoto au mke
Bi Aaisha^{ra} anasimulia kuwa, *Mtume^{saw} alikuwa akibusu (wake zake) naye amefunga. Na alikuwa akikumbatiana nao naye amefunga. Lakini yeye alikuwa akiyamiliki zaidi matamanio yake."(*Muttafiq Alaihe) katika riwaya nyingine ameongeza (Muslim) .. *katika mwezi wa Ramadhani.*

8. Kisha kama kuna moshi, vumbi, nzi, mbu au baadhi ya matone ya maji yanaingia tumboni wakati wa kusukutua lakini bila kuwa na nia basi Saumu haiharibiki. Hali kadhalika kama maji yanaingia masikioni wakati wa kuoga au mate au makohozi yanaingia tumboni bila ya nia basi Saumu haiharibiki kisha kama kuna damu inatoka kutoka meno au puani hata hivyo Saumu haiharibiki wala haiharibiki kwa kupiga mswaki kwa kutumia dawa ya meno, (mswaki uwe wa dukani yaani tooth brush au uwe wa mti) kunusa harufu, kupaka manukato, kupaka mafuta kichwani, kwenye ndevu au mwilini, kukata nywele, kukata kucha, kuoga kwa sababu ya joto kali, au kumwaga maji kichwani au kujifunika na shuka iliyo loweshwa na maji.

9. Kupiga mswaki katika Saumu.
Kuna hadithi inayopatikana katika Sahihul Bukhari, kitabus Saum kuwa, Mtume^{saw} anasema:
"*Naapa kwa Yule ambaye uhai wangu upo mkononi mwake kwamba: harufu ya kinyawani cha mfunga Saumu inampendeza Mungu zaid kuliko harufu ya misk.*"
Kuna neno la Khuluf limetumika ndani ya hadithi hii ambalo lina mana ya harufu. Harufu hii ina maana mbili:

a. Harufu inayozalika mdomoni kutokana na vipande vya chakula ambacho vinabakia humo na mswaki au brush haipigwi kwa ajili ya kuvisafisha, basi harufu mbaya huzalika wala harufu hii haijaelezwa ndani ya hadithi hii, kwani Islam inasisitiza sana juu ya usafi. Mtume^{saw} anasema: *pigeni mswaki, pigeni mswaki wala msije mbele yangu kwa meno yenye rangi ya manjano manjano.* (Kanzul Ummal) kisha Mtume^{saw} alisema akieleza sifa ya mfunga Saumu kwamba: "*kupiga mswaki ni kati ya sifa bora za mfunga Saumu*." (Ibne Majah) Mtume^{saw} alikuwa anapiga mswaki mara kadhaa katika siku moja na alishuhudiwa mara nyingi akipiga mswaki akiwa amefunga Saumu. Tooth brush (mswaki wa dukani) ni mbadala ya mswaki na saumu haiharibiki kwa kupiga mswaki uwe wa dukani (tooth brush) au uwe wa mti. Baadhi ya watu wanadhani kuwa dawa ya meno yana ladha hivyo inaharibu Saumu lakini mswaki (wa mti) pia una ladha yake..(kila mti una ladha na utamu wake kama vile muarobaini, maparachichi, mshita na mkakaya n.k.miti haya yote yana ladha tofauti tofauti) kama Saumu haiharibiki kwa mswaki huu basi haiharibiki kamwe kwa dawa ya meno pia.

b. Haruf ya aina ya pili inayotoka mdomoni si kutokana na upungufu wa usafi. Maana moja ya "khuloof" iliyoandikwa katika lugha ni *kubadilika kwa utamu wa kinywa kwa sababu ya kuchelewa kula.* (Lisanul Arab). Utamu wa kinywa unapobadilika basi harufu ya aina fulani pia inazalika…
Ina maana kuna harufu inazalika kinywani na tumboni mwa mfunga Saumu kwa sababu ya kutokula na kunywa kwa muda. Na harufu inayozalika tumboni na kufika mdomoni haina tiba wala haitoki kwa kupiga mswaki na ndio harufu iliyobainishwa ndani ya hadithi na inazalika kwa ajili ya Saumu na inampendeza Allah kwa sababu inatokana na Saumu.
(kifupisho kutoka katika Al-fazal Rabwah ya 20 July 2012 uk.7)

Kama mwanamke anapata siku zake wakati amefunga Saumu basi Saumu yake itakwisha wala hakuna kosa kwake ila Saumu hizi zitakazoachwa ni lazima zitimizwe baadaye.

Katika hali ya saumu mtu anaweza kuoga, kupiga mswaki na kupaka manukato (Bukhari).

Mwanamke anaweza kuonja chumvi katika chakula kwa ulimi tu, asiimeze.

Katika usiku wa saumu mtu anayo ruhusa kuingiliana na mkewe (Kurani).

Mambo Ambayo Yanavunja Saumu

- Kama mtu yeyote anakula maksudi au kufanya tendo la ndoa hali amefunga basi Saumu yake inabatilika.
- Kupigwa sindano au kujitapisha pia ni mambo yanayoharibu Saumu.
- Na kama yeyote anaharibu Saumu yake kwa maksudi basi atapewa adhabu pamoja na kurudia tena ile Saumu. Adhabu yake ni kufunga siku sitini mfululizo na kama hawezi, awalishe maskini sitini kwa pamoja au maskini mmoja mmoja au kumpa maskini moja nafaka ya siku sitini au kumlipa pesa sawa na hesabu yake.
- Lakini kama mtu yeyote anafungua Saumu kwa kosa bila ya kuwa na nia basi hana dhambi ila ataifidia na kuitimiza katika siku nyingine. Katika hali ya saumu mtu hana ruhusa kuvuta sigara au kunusa tumbaku au kuitia mdomoni.
- Kisha mambo ya upuuzi yaani kusikiliza muziki, kutazama filamu, au matumizi mabaya ya mtandaoni pia yanapunguza thawabu ya Saumu hivyo lazima tujiepushe navyo na vingenevyo vingi.

Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa na Seyyedna Ahmad^{as}

1. Swali liliulizwa kwamba je, inajuzu kuweka dawa katika jicho la mfunga saumu linaloumwa?
Alisema: Swali hili si sahih. Amri ya kufunga Saumu haimhusu mgonjwa.

2. Swali liliulizwa kuwa, mtu asiyeweza kufunga Saumu, anatakiwa kumlisha maskini mmoja. Je inajuzu kutuma pesa za chakula kile katika fungu la mayatima hapo Qadian.
Alijibu: ni sawa tu hata kama anamlisha maskini mjini mwake au anatuma katika fungu la mayatima.

3. Swali liliulizwa kuwa je, mfunga Saumu anaweza kupaka wanja au la?
Alisema: Ni makrooh(haipendezi) na kuna haja gani ya kupaka wanja wakati wa mchana. Anaweza kupaka wanja usiku. (Malfoozat J.5.uk.135)

Inaendelea uk. 11

Fiqh ya Ramadhani

Inatoka uk 10

Namna ya kulipia Saumu za Ramadhani zilizopotea

Saumu za Ramadhani zilizopotea kwa udhuru wa ugonjwa au safari, lazima zitimizwe hesabu zao baadaye lakini si lazima zifungwe mfululizo. Zinaweza kufungwa kwa kuacha siku moja moja jinsi anavyopenda.
(Fiqha Ahmadiyya J.1.UK. 301)
Saumu sita za Shawwali pia si lazima zifungwe mfululizo bali zinaweza kufungwa kwa siku moja moja ndani ya mwezi wa Shawwali.
Hukumu ya Kufunga kwa Nchi Maalum
Katika nchi ambazo mchana ni mkubwa sana hadi masaa 22 au 23 wafungaji wa nchi hizo wapange muda wao wa kula daku na kufuturu kwa kutumia majira ya nchi za jirani, vinginevyo hakutokuwa na muda wa daku, wala futari, wala muda wa Tahajjud, Sala ya Alfajr au Sala ya Isha.

Sadaka ya Fitri

Mtume^{saw} amewaagiza Waislamu wote wanawake kwa wanaume, Watu wazima kwa Watoto wachanga (hata wale waliozaliwa kabla kidogo tu ya sala ya Idi), watoe sadaka ya fitri, kiwango chake kimeelezwa katika hadithi za Mtume^{saw} kuwa "Sa'a moja, iliyokuwa sawa sawa na kilo tatu, lakini maskini na wasio na uwezo watatoa nusu. Sadaka hii hupelekwa kwa mkubwa wa Waislamu kabla ya siku ya Idi na kugawa mapema ili nao wajinunulie nguo mpya na kujifurahisha katika siku kuu ya Idi.

Maagizo ya Mtume^{saw} Kuhusu Fitri

1. Hazrat Abdullah bin Omar^{ra} anasema: *Mtume^{saw} amewalazimisha Waislamu kutoa "sa'a" moja ya tende au sa'a moja ya Shayiri kama sadaka ya Fitri, akiwa mja kazi au mwenye huru, akiwa mwanume au mwanamke, akiwa mkubwa au mdogo, na Mtume^{saw} aliamuru kuwa (fitri) itolewe kabla ya kutoka kwa ajili ya sala ya Idi.* (Sahihul Bukhari Kitabuz Zakat)
2. Hazrat Ibne Abbas^{ra} anasimulia kuwa *Mtume^{saw} aliweka sadaka ya fitri kwani inamtakasa mfunga saumu na upuuzi na uchafu na kuwapa maskini chakula. Anayeitoa kabla ya sala ya Idi basi hupokelewa (kama sadaka ya fitri) na atakayeitoa baada ya sala basi itakuwa sadaka ya kwaida tu (yaani sio fitri tena).* (Abu Dawood Kitabuz Zakat)

Jumuiyya yetu inafuata njia hizo zote mbili za kutoa sadaka ya Fitri kwamba wenye wasa hutoa thamani ya sa'a moja ama wengine wasioweza wanatoa sawa na nusu ya sa'a juu ya kila kichwa. Sadaka ya Fitri lazima itolewa kwenye Jamaati wala hairuhusiwi kutoa mwenyewe kwa maskini yeyote na popote.
Sadaka ya Fitri inakuwa wajibu mara baada ya kuandama kwa mwezi wa Ramadhani ila inaruhusiwa kutoa hadi kabla ya kutoka kwa ajili ya sala ya Idi. Ni bora itolewe mapema ili ifike kwa wenye kustahili kabla ya Idi na wao waweze kujianda na kushiriki katika furaha ya Idi.

Ramadhani na Maombi



Allah Anasema Akieleza umuhimu na haja ya kuomba dua kuwa: *Sema: Mola wangu Hangewajalini kama si kuomba kwenu.*
Kisha Anasema Mungu Mtukufu: *"Na Mola wenu Husema: Niombeni nitawajibuni. Kwa hakika wale wajivunao kufanya ibada Yangu, wao bila shaka karibuni wataingia Jahannamu wakifedheheka."* (Sura Almumin 40:61)
Hazrat Khalifatul Masih wa Kwanza wa Seyyedna Ahmad^{as} anasema: *"Mtu hupata Ukaribu na Allah (ndani ya Ramadhani). Allah Mtukufu Anasema, Ninakuwa karibu zaidi na kuyapokea maombi.*
Si maana yake kwamba mpatapata kile chote mtakachoomba kwa sababu Ameshaeleza mahala pengine, katika sura Al-Anaam (aya:42). "kama Akitaka Ataondoa shida ile…"
Amesema, *"jinsi mtaendelea kuwa watiifu wangu na kuongezeka katika Imani basi kiasi kile tu Nitapokea maombi yenu."* (Haqaiqul Furqan, J.1.UK.308)
Hazrat Abu Hurairah^{ra} anasimulia kuwa: *"Mjumbe wa Allah^{saw} alisema; yule anayetaka kuwa Mungu Amsikilize katika nyakati za shida na taabu, basi mtu huyu amwombe sana katika hali ya raha."* (Tirmizi Abwabu adawati, Babu Dawatul Muslimi Mustajabatun
Mtume^{saw} anasema pengine kwamba: *"Mtu anakuwa karibu mno na Mola wake anapokuwa katika sujuda. Basi ombeni sana katika sujuda."* (Muslim Kitab us Salat)
Imesimuliwa na hazrat Abdillahi ibne amri ibne Al-aasi^{ra} wanasema: Mtume^{saw} alisema; *Kwa yakini dua ya mfunga saumu haikataliwi, anayoiomba wakati wa kufuturu.*
Hazrat Mirza Masroor Ahmad Khalifa wetu wa Tano^{atba} anasema: *"Basi saumu hizi ni chanzo cha kupata ukaribu naye na sababu ya kupokelewa kwa Maombi. Hivyo basi ni jukumu la kwetu sisi kwamba tumuombe Mungu kwa uyenyekevu mkubwa na kumlilia sana. Lakini tukumbuke kila siku kwamba tusimuombe juu ya shida, haja na kusudio letu la kidunia tu bali tumuombe ridha yake. Ridha yake nini?* Anasema*: "Basi inatakiwa watikie kauli yangu na kuniamini Mimi."*
Kutikia kauli yake Mungu ndio kufuata maamrisho yake. Anasema*: Ninajibu dua ya muombaji anaponiita Mimi. Ombi hili litapokelewa wakati ule tu ambapo tutajitahidi kupata maendeleo ya Imani….yaani maombi yatakubaliwa pale tu ambapo tutajisogeza katika kupata maendeleo ya Imani na maendeleo ya Imani itakuwepo pale tu ambapo tutatia bidi katika kutii maamrisho ya Allah Mtukufu kwa uaminifu na kujitahidi kufanya ibada yake (Mungu)."* (Khutbate Masroor J.6.UK.363)
Imam uz zaman, seyyedna Ahmad^{as} anasema: *"Mwezi wa Ramadhani ni mwezi wenye mibaraka. (na) Mwezi wa (kuomba sana) maombi."* (Malfoozat J.1.UK.439)

Allah Atuwezeshe kwa ajili ya kufanya maombi ambayo kwayo tunaweza kujisafisha vizuri na kujitakasa mno ili tuwe miongoni mwa watumishi wake ambao wanapata ukaribu na Allah Mtukufu na maombi yao yanakubaliwa kila siku. Aamiina.

Dua Kubwa Zaidi, Kumsalia Mtume^{saw}

Dua muhimu mno inayookelewa moja kwa moja na kuleta baraka na heri nyingi kwa ajili ya muombaji ni sala ya Mtume^{saw} yaani kumsalia Mtume Mtukufu^{saw} nasi tumehimizwa ndani ya Qurani Tukufu kuhusu jambo hili. Allah Anasema: *"kwa yakini Allah na Malaika wake wanamrehemu Mtume^{saw} Enyi mlioamini! Ninyi nanyi msalieni (kumsalia Mtume^{saw} ni kumwombea dua ya kupata amani, rehema na baraka) na mwombeni amani sana.* (Sura Alahzab 33:57)
Imesimuliwa na Hazrat Aamir bin Rabiah^{ra} ya kwamba Mtume^{saw} alisema: *"Mwislamu yeyote anisaliaye, basi Malaika huendelea kumsalia kwa wakati wote atakao kuwa ananisalia. Sasa akipenda anaweza kuzidisha."*
Imesimuliwa na Hazrat Fudhalah bin Ubaid^{ra} kwamba *Mjumbe wa Allah^{saw} alimsikia mtu mmoja akiomba dua katika sala yake. Mtu huyu hakumtukuza Allah wala hakumsalia Mtume^{saw}. Hapo Mtume^{saw} alisema: huyu amefanya haraka. Kisha akamwita na kumwambia yeye ama mwingine: mmoja wenu anapoomba dua inampasa aanzie na kumhimidia Mola wake na kumsifu kisha amsalie Nabii^{saw}. Kishapo aombe baadaye apendavyo.* (Abu Dawood kitabus Salat Babu dua)
Hazrat Masihe Maud^{as} anaeleza uzoefu wake binafsi wa baraka za kumsalia Mtume^{saw} akisema: *ilitokea hivi wakati fulani kwamba, nilishugulikia sana kumsalia Mtume^{saw} kwa siku nyingi sana kwa kuwa nilikuwa na yakini kwamba njia za Allah ni nyembamba sana, bila ya kumpitia Mtume^{saw} haziwezi kupatikana, kama vile hata Allah Anasema: na mtafute njia kwake. (Al-Maida 5:36)*
Basi baada ya muda Fulani nikaona katika hali ya kashfi kwamba wachukuzi wawili wa maji wamekuja, mmoja akaingia nyumbani mwangu kwa mlango wa ndani na mwingine kwa mlango wa nje, walikuwa wamebeba mabegani mwao viroba vya nuru wakasema:
baraka hizi ni kwa sababu ya wewe kumsalia Muhammad^{saw}.(R.Kh.J.22. UK.131 maelezo ya chini)
Hazrat Aqdas Masihe Maud^{as} anasema: *"kwa sababu ya sala ya Mtume^{saw} …naona baraka za Allah zinaelekea kwa Mtume^{saw} kwa sura ya ajabu ya nuru na halafu bbada ya kufika huko zinapenya ndani ya kifua cha Mtume^{saw} na baada ya kutoka humo zinageuka kuwa mifereji mingi isiyohesabika na zinamfikia kila anayestahili kuzipata kwa kiwango chake. Kwa yakini hakuna baraka iwezayo kufika kwa watu wengine bila ya kupitia kwa Mtume^{saw}. Sala ya Mtume ni nini? Ni kuitikisa arshi ile ya Mtume^{saw} ambamo yabubujika hiyo mifereji ya nuru. Yule anayetaka kupata baraka na Fadhili za Allah yamlazimu amsalie sana Mtume^{saw} ili baraka hiyo ipate kutikisika.* (Al-Hakam, 28 Feb.1903.uk.7)
Hivyo basi sisi sote tunatakiwa kumsalia sana bwana wetu mpendwa Mtume^{saw} ili tupate rehema, baraka na heri nyingi za Ramadhani.
Hazrat Ubaiyi bin Kaab^{ra} anasimulia kuwa, mimi nilimuelezea Mtume^{saw} kwamba, natumia sehemu kubwa ya maombi yangu katika kumsalia Nabii^{saw} ni bora kama Huzur^{saw} mwenyewe aniambie kuwa, nitumie muda gani kati ya muda wa maombi yangu katika kumsalia Nabii^{saw}. *Mjumbe^{saw} alisema kadri unavyopenda. Nilisema je, robo ya muda? Alijibu jinsi unavyotaka, kama unaweza kuuzidisha basi itakuwa bora zaidi kwako. Nilimuuliza je, nusu ya muda? Alisema jinsi upendavyo, na kama unauongeza basi ni bora zaidi. Nilimuomba je, thuluthi mbili? Alijibu jinsi uwezavyo, kama utaongeza humo basi itakuwa bora kabisa. Nilisema naweka muda wote wa maombi yangu kwa ajili ya kumsalia Mtume^{saw}. Mtume^{saw} alisema basi ndipo taabu na huzuni yako yote yataondoka kwako na madhambi yako yote yatasamehewa.* (Timizi Abwab sifa ya Kiyama)
Khalifa wetu wa Tano Hazrat Mirza Masroor Ahmad^{atba} anasema: *"Allah Amesisitiza sana waaminio kuhusu kumsalia Mtume^{saw} kuna nini sababu yake? Je Mtume^{saw} anahitaji maombi yetu? Hapana (hana haja). Bali tumefundishwa njia hii kuwa: Enyi watumishi wangu! Mnaponiletea haja zenu, mnapofika kwangu, ili maombi yenu yapokelewe na kutimizwa kwa haja zenu, basi mna (weza kutumia) njia moja tu nayo ni hii kwamba mufike kwangu kupitia Mtume wangu^{saw}. Kama hamtatumia njia hii basi ibada zenu zote zitapotea bure kwani vitu hivi vyote, ulimwengu huu wote nimeviumba kwa ajili ya Mtume huyu mpendwa wangu^{saw}.*
(Khutbate Masroor J.1.UK.288)
Kama imeelezwa katika hadithi kuwa: Allah Anasema: *"kama nisingekuumba wewe basi nisingeumba ulimwengu huu"* (Mauzuate Kabiir uk.325)

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

SHAB.-RAMADH. 1442 AH | APRILI 2021 | SHAHADAT 1400 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

Atakayefunga saumu siku yoyote basi asiingiliane wala asitukane ama kuongea upuuzi. Na kama mtu mwingine amtukane na kutaka kupigana naye basi aseme mimi nimefunga saumu (**Sahihi Bukhari na Muslim**)

Kumi la Mwisho na Itqaf



Bwana wetu mpendwa Mume^{saw} alisema kuhusu mwezi wa Ramadhani kwamba:

"Huu ndio mwezi ambao mwanzo wake ni rehema na kati yake ni wakati wa msamaha na mwisho wake ni muda wa kupewa ujira kamili yaani kuepushwa na moto."

Hazrat Aaisha^{ra} anasimulia kuwa; *Mtume^{saw} alikuwa, linapoingia kumi la mwisho la Ramadhani akijifunga kibobwe (kutia bidii na jitihada katika ibada na) kuhuisha usiku na kuwaamsha wake zake.* (Sahih Bukhari na Sahih Muslim)

Mtume^{saw} alisema akieleza baraka za kumi la mwisho la Ramadhani kwamba:

Usiku wa mwisho wa Ramadhani ni usiku wa ghofira (msamaha) kwa ajili ya umati wangu. Mtume^{saw} aliulizwa kuwa ewe Mjumbe wa Allah! je, usiku wa mwisho wa Ramadhani unakuwa "lailatul Qadri" (usiku wa heshima)? Alisema: hapana! bali mfanya kazi anapomaliza shuguli zake basi wakati ule analipwa ujira wake. (na huu ni ujira wa msamaha). (Musnad Ahmad Bin Hanbali)

Ndugu wasomaji! Tunapaswa kufuata kikamilifu desturi hii ya kutia bidi katika ibada zetu zote za namna mbali mbali katika siku hizi kumi za mwisho.

Ibada ya Itikafu

Allah Anasema: "*Na hali mnakaa msikitini.*" Kilugha maana ya Itikafu ni kuketi sehemu au kujifungaia mahala. Na sawa na istilahi ya Kiislam ni kuketi msiktini kwa nia ya ibada katika hali ya kufunga saumu.

Imeandikwa katika kitabu kinachoitwa Hidaya kuwa: "*kuketi msikitini kwa saumu na kwa nia ya ibada ni Itikafu.*" (Hidaya babul Itikaf)

Qurani Tukufu imetuelezea kuwa itikafu ilikuwepo katika dini zingine pia zilizotangulia kama saumu;

"Tuliwaagiza Ibrahimu na Ismaili kwamba ninyi wawili mwitakase Nyumba Yangu kwa ajili ya waizungukao na kwa wakaao na kwa wanao rukuu na kusujudu."(Albaqrah 2:126)

Hazrat Aaisha^{ra} anasimulia kuwa; Mtume^{saw} alikuwa akiketi Itikafu kumi la mwisho la Ramadhani mpaka Allah Akamfisha. Kisha wakeze wakaketi Itikafu baada yake. (Bukhari na Muslim)

Mtume^{saw} alipotaka kuketi Itikafu, alisali Al-Fajiri kisha akiingia mahala anapofanya Itikafu. (Muttafiq alaihe)

Hazrat Musleh Maud^{ra} anasema:

"Tunaketi Itikafu asubuhi ya tarehe 20, zinakuwa siku 10 na muda mwingine zinakuwa 11."

(Al-Fazal ya tarehe 3 Novemer 1914)

Mwenye kuketi Itikafu anatakiwa kukaa na kushinda wakati wote katika mahala pake, ulioandaliwa kwa ajili yake akijishugulisha katika kukumbuka Allah, kufanya ibada, kusali sala za nafali na kusoma Qurani Tukufu.

Imesimuliwa na Hazrat Aaisha^{ra} kwamba: *Sunna kwa anayeketi Itikafu ni kuwa, asimtembelee mgonjwa, wala asihudhurie mazishi, wala asimguse mwanamke, (kwa jimai). Wala asitoke ila kwa dharura, isipokuwa katika jambo ambalo halina budi. Wala hakuna kuketi itikafu isipokuwa kwa saumu, wala hakuna kuketi itikafu ila katika msikiti wa Jamia (unaposaliwa Ijumaa na sala kwa jamaa).* (Abu Dawood)

Hazrat Musleh Maud^{ra} anasema; *Inawezekana kuketi Itkafu nje ya msikiti ila haitakuwa na thawabu ile inayopatikana kwa kuketi msikitini.*

(Alfazal ya tarehe 6 Machi 1962)

Mwanamke pia anaweza kuketi Itikafu msikitini lakini ni bora zaidi kuchagua sehemu maalum kwa ajili ya kusali nyumbani mwake na kuketi Itikafu humo, imeandikwa hivi: "*ama mwanamke basi aketi Itikafu katika msikiti wa nyumba yake.*"

Hairuhusiwi kutoka nje ya msikiti baada ya kuketi Itikafu isipokuwa kwa ajili ya mahitajio ya lazima kama haja ya lazima ya ubinadamu, kuchukua Udhuu, na kuoga kwa janaba. Kwa ajili kuoga kwa janaba ni lazima aende kuoga hata nje ya msikiti kama hakuna bafu kwenye eneo la msikitini hali kadhalika mwanamke akipata hedhi (siku zake) ndani ya Itikafu basi aache Itikafu na asikae msikitini tena.

Mwenye kuketi Itikafu ajihusihe na ibada na kumkumbuka Allah Mtukufu kwa wingi, asipoteze muda katika mazungumzo ya kawaida tu wala haifai pia kukaa kimya kabisa kwa sababu hakuna saumu ya kushinda na kutokusema.

Bwana wetu Mpendwa Mtume^{saw} alisema: *"Mwenye kuketi Itikafu anajiweka kikamilifu mbele ya Allah na kusema, e Mola wangu! Naapa sitatoka humo mpaka Unirehemu".* (Durre Mansoor)

Kisha alisema pengine akieleza fadhila yake kuwa:

"Anayeketi Itikafu siku moja akitafuta ridha ya Allah- Allah Ataweka handaki (pango) tatu baina yake yeye na Jahannamu na umbali wa kila handaki utakuwa mkubwa zaidi kuliko umbali wa Mashariki na Magharibi. (Durre Mansoor)

Bwana wetu Mtume Mtukufu^{saw} anasema kuhusu baraka za Itikafu kuwa: "*anayeketi Itikafu siku kumi katika Ramadhan (akizingatia masharti) atakuwa na thawabu ya Hijja mbili na Umra mbili.*"

Khalifa wetu wa tano, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad^{atba} anasema:

Allah Humuelekea Mja wake zaidi kuliko awali katika kumi la mwisho. Hudhihirisha matukio mengi zaidi ya kuyapokea maombi kuliko awali…. Mjumbe wa Allah^{saw} alisema kuwa siku hizi za kumi la mwisho ni siku za kuepushwa na Jahannamu kwa sababu ya mwezi huu wenye mibaraka. Mtenda dhambi mkubwa pia kama akimuelekea Allah basi atakuwa mwenye kujilinda na moto. (Khutbate Masroor J.3.UK.640)

Allah Atuwezeshe sisi sote kwa ajili ya kutekeleza vyema wajibu wetu uliojuu yetu kuhusu ibada hii tukufu wa kuketi Itikafu ndani ya Ramadhani kila mwaminio atafute muda wa kukaa Itikafu mara kwa mara kwenye Maisha yake na wale wanaokosa nafasi basi wajaribu kuketi Itikafu angalau mara moja tu.

Lailatul Qadri

Allah Anasema Akieleza umuhimu na baraka za Lailatul Qadri kwamba:

"Hakika Tumeiteremsha (Qurani) katika usiku wa heshima. Na nini kitakujulisha usiku wa heshima ni nini?

Usiku wa heshima ni bora kuliko miezi elfu. Huteremka Malaika na ufunuo katika huo kwa idhini ya Mola wao kwa kila jambo. Amani na (usiku) huo (unaendelea) mpaka mapambazuko ya Alfajiri. (Suratul Qadri Aya 1-6)

Mtume wetu Mtukufu^{saw} alisema juu ya ubora wa ibada ya usiku huu kuwa:

"Atakayesimama kufanya ibada ya (usiku wa) Lailatul Qadri kwa uaminifu wa Imani na kwa nia ya kupata thawabu, atasamehewa madhambi yake yote, ya mwanzo na ya mwisho na atakaye funga saumu ya Ramadhani akiwa na Imani kwa nia ya kupata thawabu, madhambi yake yote yatasamehewa yaliyotangulia." (Bukhari Kitab us Saum)

Khalifa wetu wa Tano hazrat Mirza Masroor Ahmad^{atba} anasema kuhusu usiku huu wa heshima kuwa: *"Maana ya Lailatul Qadri ni usiku ule ambamo hukadriwa bahati ya mtu. Na hufanyiwa uamuzi kwamba atatendewa vipi kwenye mwaka ujao? Atakuwa kiasi gani, na kupata maendeleo gani, na manufaa gani gani? Na kupata hasara gani? Maamuzi yote ya maendeleo ya binadamu hafanyika katika Lail yaani muda wa giza….tunapatakujua kupitia sehemu moja ya Qurani kuwa maendeleo ya kimwili ya binadamu pia huwa unapatikana kupitia giza kadhaa mfululizo. Kuzaliwa kwa mtoto, tumboni mwa mama ni mjumuiko wa giza kadhaa na humo humo hufanyika maamuzi ya maendeleo ya kimwili ya binadamu…. hivyo basi kama maendeleo ya kimwili yanapatikana gizani hali kadhalika maendeleo ya kiroho pia yanafanyika ndani ya usiku."* (Hotuba ya Ijumaa ya tarehe 25 Julai 2014)

Seyyidna Ahmad alisema akieleza maana za Lailatul Qadri kuwa: *"..hapo kuna maana tatu za Lailatul Qadri.*

***Ya kwanza** ni hii kuwa kuna usiku wa Lailatul Qadri, unaopatikana katika Ramadhani.*

***Ya pili** ni hii kuwa, zama za Mtume^{saw} pia zilikuwa Lailatul Qadri. Yaani yeye^{saw} alikuja katika wakati wa ujinga mkubwa na kwenye giza la kutokuwa na Imani na Malaika walishuka, kwani Nabii haji duniani peke yake bali anakuwa mfalme na pamoja naye linakuwepo jeshi la Malaika malukuki au mamillioni, amabo hujishugulisha na kazi yao na kuvuta mioyo ya watu kwenye wema.*

***Ya tatu,** (kupatikana kwa) muda mzuri na msafi kwa ajili ya mtu ni Lailatul Qadri (kwake). Muda wote hauwi sawa. Baadhi ya wakati, Mtume^{saw} alikuwa anamwambia Bi Aaisha^{ra} kuwa: …..E Aaisha unitulize na kufurahisha, na muda mwingine alikuwa (saw) anazama kabisa katika dua."* (Malfoozat J.1.UK.536.)

Njia bora zaidi ya kupata Lailatul Qadri ni hii kwamba: Mwaminio aendelee kufanya maombi mwezi mzima wa Ramadhani na kufunga saumu ya Ramadhani kwa uaminifu wa Imani kisha Allah Anaweza kumdhihirishia Lailatul Qadri kwa namna yoyote.

Allah Atujaalie kila mmoja wetu Lailatul Qadri anayejitahidi katika Ramadhan kwa ajili ya kuupata usiku huu. Aamiina.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com